

**WEZI** waua mtoto wakisaka fedha za TASAF alizopewa mama yake mzazi

UKURASA 18

**SONGWE** yatajwa kuathirika biashara haramu binadamu

UKURASA 3


NIPASHE JUMATATU JULAI 10, 2023

Nipashe Spotika

WACHEZAJI 10 WA THAMANI ZAIDI DUNIANI KWA SASA 12 - 13

WILLIAM SALIBA

MABEKI WATATU ARSENAL WANAOWEZA KUWEKWA BENCHI NA JURRIEN TIMBER

LONDON, England

KWA mujibu wa Fabrizio Romano, mazungumzo kati ya Arsenal na Ajax kuhusu uwezekano wa kumsajili Jurrien Timber yanakaribia kukamilika. Ameeleza kuwa ada ya uhamisho inaweza kupanda hadi euro milioni 47.

Timber mwenye umri wa miaka 22, ni beki chipukizi anayetumainiwa na uwezo wake wa kufanya mashambulizi muhimu ni bora.

Ustadi wake wa kuendeleza mpira katika mashambulizi pia ni sifa nyingine muhimu ambayo anayo. Katika msimu wa 2022-23, alishinda asilimia 76.2 ya safu yake ya ulinzi na pia alisajili mchango wa mabao manne katika michezo 47.

'Washikabunduki' wanamsajili Mholanzi huyo kwa sababu ya uwezo wake wa kucheza kama beki wa kati na beki wa kulia inapobidi, jambo ambalo ni la ushindi kwa klabu. Mtindo wake wa uchezaji unalingana kabisa na muundo wa kocha Mikel Arteta.

Hata hivyo, kupatikana kwake kunaweza kumaanisha kuwa baadhi ya mabeki wa kati waliopo klabuni hapo wanaweza kuondoka au kuachwa benchi. Acha tuangalie wachezaji watatu ambao wanaweza kuathiriwa ikiwa mpango huo utakamilika...

**#1. Ben White**

Beki hodari ambaye anaweza kuathiriwa na uhamisho huo ni Ben White, kwani ndiye chaguo la kwanza la beki wa kulia wa Washikabunduki hao msimu uliopita.

Wakati wa msimu wa 2022-23, White alifunga mabao mawili na alitoa pasi tano za mabao katika mechi 46 kwenye mashindano yote.

Hata hivyo, kutokana na Timber kuingia kwenye mpambano huo, nafasi yake ya kucheza kama beki wa kulia inaweza kupungua.

Hii inakuja kutokana na ustadi wa Timber kucheza kwenye beki ya kulia pia. Inaweza pia kusemwa kuwa Timber ana ufundi zaidi na wa kutisha katika beki ya kulia kuliko White. Kwa hiyo, wakati wake wa kucheza unaweza kupungua msimu ujao.

**#2. Jakub Kiwior**

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Poland ni beki bora wa kati, na uwezo wake wa kumkaba mpinzani wake katika safu ya ulinzi ni wa ajabu. Zaidi ya hayo, nafasi yake katika ulinzi ni ya hali ya juu pia.

Januari 2023, Washikabunduki walimsajili kutoka Spezia kwa pauni milioni 20, na alicheza mechi nane, na kusaidia kusawazisha mabao mawili kama mchezaji wa Arsenal msimu uliopita.

Ingawa inaweza kutabiriwa kuwa Kiwior ni beki wa kati anayetarajiwa, kuwasili kwa Timber kunaweza kumuacha benchi.

**#3. William Saliba**

William Saliba ni mmoja wa wachezaji bora zaidi wa msimu wa 2022-23, na ustadi wake wa ulinzi uliboresha utendaji wa jumla wa Arsenal pale nyuma.

Mfaransa huyo alicheza mechi 33 kwenye mashindano yote akiwa na Arsenal msimu uliopita. Hata hivyo, beki huyo anayetumia mguu wa kulia alijitahidi kubaki fiti, kwani alikuwa nje ya uwanja kwa mechi 12 mwishoni mwa msimu uliopita.

Kwa kuzingatia kiwango cha Saliba msimu uliopita na umuhimu wake kwa timu, kuna uwezekano mdogo wa Timber kumtoa kwenye kikosi cha kwanza. Hata hivyo, itakuwa ya kuvutia kuona uamuzi wa kocha utakuwa nini ikiwa Saliba atajitahidi kubaki fiti.

**ISIKUPITE**

KWA mujibu wa mtandao wa ESPN, Bukayo Saka wa Arsenal ndiye winga bora zaidi akifuatiwa na Khvicha Kvaratskhelia (Napoli), Jack Grealish (Man City), Ousmane Dembélé (Barca), Gabriel Martinelli (Arsenal), Riyad Mahrez (Man City), Kingsley Coman (Bayern), Rodrygo (Madrid), Phil Foden (Man City) na Moussa Diaby (Leverkusen).

UKURASA 11

Jumatatu Julai 10, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581367

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Kilichojificha matukio ya watoto kujinyonga

**WATAALAMU** saikolojia, viongozi wa dini wataja sababu zinazoshtua... *Endelea ukurasa 2*




Ndege mpya ya mizigo ya ATCL ikipakia mizigo kwa ajili ya kuanza safari za nje ya nchi kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mwinyi ataka Afrika iongeze nguvu vita kuikabili rushwa

UKURASA 18

## Ndege mpya mizigo ATCL yaanza safari

UKURASA 4

**MICHEZO** **AZAM YAPAA TUNISIA KUANZA KAMBI** UK. 23

**KATUNI** UK. 6




Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Epvate and Fortune International Consulting (EFIC), Peter Mapigano (kulia), akichangia mada ya "Utumishi wa Umma Unaoweka Watu Mbele" wakati wa kongamano la Rasilimali Watu lenye lengo la kutoa mafunzo kwa waajiri na waajiriwa lililofanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Wengine kutoka kushoto ni Balozi Peter Kallage; Mkurugenzi wa Huduma wa Mamlaka ya Anga (TCAA), Teophory Mbilinyi na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Uongozi Institute, Kadari Singo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wataalamu wafichua kilichojificha matukio ya watoto kujinyonga

**Na Jenifer Gilla**

KATIKA siku 12 zilizopita, kuna matukio matatu ya watoto kudaiwa kujinyonga nchini. Sababu za uamuzi huenda zisiwe na maana kwa mtu mzima, labda kwa watoto kutokana na uwezo mdogo wa kufikiri.

Wasaikolojia tiba na malezi wamesema kukosa malezi ya wazazi ni sehemu ya mambo yanayoweza kusababisha watoto kujiua - wanakosa mahitaji yao ya kihisia na stadi nzuri za kutatua matatizo yao ikiwamo uvumilivu, kujiamini na subira.

Wataalamu hao pia wamesema wazazi au walezi wanapopuuza mahitaji madogo ya watoto ambayo huendana na umri wao na kuwatimizia makubwa ambayo hayana msaada kulingana na umri wao, ni sababu nyingine inayoweza kuchangia uamuzi huo wa kujiua.

Mtazamo huo umeangaziwa na mwandishi baada ya kuripotiwa kwa matukio ya hivi karibuni ya watoto kudaiwa kujitoa uhai kutokana na sababu mbalimbali.

Yanaporejewa matukio matatu yaliyoripotiwa ndani ya siku 12 zilizopita kuanzia Juni 27, yanajumuisha la mwanafunzi wa darasa la tano katika Shule ya Msingi Mother Kelvin iliyoko Wilaya ya Same, mkoani Kilimanjaro, Alex Mgonja, alidaiwa kujinyonga kwa madai ya kukataliwa kupanda basi la shule wiki iliyopita.

Juni 27, mwanafunzi wa darasa la nne katika Kijiji cha Ikengwa, mkoani Dodoma, Zamada Jafari (13) alifariki dunia baada ya kudaiwa kujinyonga kwa kutumia mtandio, chanzo kikidaiwa kukosa nguo ya sikukuu.

Tukio lingine ni Jafari Mwashitete, mwanafunzi wa kidato cha tatu katika Shule ya Sekondari Lumbira ya wilayani Mbozi, mkoani Songwe, anayedaiwa kujinyonga kwa kutumia tai huku akidaiwa kuacha ujumbe kwamba uamuzi huo wa kujitoa uhai umetokana na kutofurahishwa na kitendo cha wazazi wake kumhamishia katika shule hiyo.

**WATAALAMU WANENA**

Msaikolojia tiba, Dk. Saldeen Kimangale, kutoka Hospitali ya Somedics Polyclinic Health Centre ya jijini Dar es Salaam, alisema hivi karibuni kumekuwapo na matukio mengi ya watoto wadogo kukatisha uhai wao kwa sababu ambazo katika hali ya kawaida mtu hawezi kuchukua uamuzi kama huo.

Alisema ufuatiliaji wake umebaini watoto wengi wanaoripotiwa kujiua, hawaishi na wazazi wao, bali walezi ikiwamo bibi, babu na shangazi.

Mtaalamu huyo analitaja ni jambo linalosababisha watoto kukosa mahitaji yao ya kihisia kama inavyostahili, kukosa njia bora za kuwasilisha mahitaji yao na kukosa stadi nzuri za kutatua matatizo yao kama vile subira, uvumilivu, ujasiri na kujiamini.

Vilevile, aliwanyooshea kidole wazazi na walezi wengi wana majibu mepesi kwa mahitaji madogo ya watoto wao na kutimiza mahitaji makubwa ambayo wakati mwingine siyo ya msingi kulingana na umri wa mtoto.

"Kwa mfano, pipi kwa mtoto wa miaka minne au mitano ni bora sana kuliko simu ya iPhone 13. Sasa mzazi badala ya kumpatia mtoto pipi anayoihitaji anampa iPhone," alifafanua.

Msaikolojia tiba huyo alisema hali hiyo wakati mwingine inasababishwa na wazazi kutowasikiliza na kuyafanyia kazi mahitaji na changamoto wanazopitia watoto wao na kuyachukulia kama jambo la kawaida kwa kuwa tu haijawatokea wao au iliwatokea na wakakabiliana nayo.

"Jambo lisilokuwa la maana au jambo la kawaida kwako wewe mtu mzima au tu mtu mwingine, huenda likawa muhimu sana kwa mtoto au mtu mwingine.

"Dhana hii imefanya tunayapuuza mahitaji ya msingi sana ya watoto wetu na hitaji kubwa kuliko yote ni kusikilizwa kwa umakini na kuelewa kile walichokusudia na kisha kukifanyia kazi," alisema Dk. Saldeen.

Mtaalamu huyo pia alitaja sababu nyingine ni wazazi kutofuatilia mienendo na hisia za watoto wao. Anasema ni tabia inayochangia matukio ya kujiua.

"Mpaka mtoto anafikia hatua ya kujitoa uhai wake, alishafanya majaribio kadhaa ya kufanya tukio kama hilo huko nyuma," alisema.

Dk. Saldeen anashauri wazazi na walezi wawe na muda wa kukaa na watoto wao kusikiliza mahitaji yao na wawasaidie kufurahia utoto wao bila kuingiliwa na kupewa bughudha.

"Wazazi wajitahidi kuwatimizia watoto wao mahitaji yao ya msingi bila kupuuza, na pale panapokuwapo na ugumu, washirikishe watoto ili wasijenge dhana kuwa wamepuuzwa, wamekataliwa au hawana thamani au hawapendwi," alisema.

Msaikolojia tiba huyo pia anashauri watoto wajengee uwezo kifikra na kufundishwa stadi mbalimbali za maisha ikiwamo kuwasiliana katika kuleta maana, stadi za kutatua matatizo na stadi za kukabiliana na msongo wa mawazo badala ya kuacha majukumu hayo kwa shule.

Mchungaji mstaafu wa KKKT, Richard Hananja, aliwataka wazazi na walezi kulea watoto wao katika misingi ambayo itawaondolea utegemezi ili kutengeneza kizazi ambacho kisichokata tamaa na kupambana na maisha hata pale wazazi wao watakapokuwa hawapo duniani.

"Kwa hiyo, sisi tunapanda nini? Watu wengi sasa wanatunza na sio kulea. Tunamwachia nini mtoto yule hata leo unapoondoka duniani? Unamwachia nini?

"Anaachiwa hali ya kujitegemea, kuona kuwa hata wazazi wakiwa hawapo wanaweza kuishi? Macho yake yanaona ushindi au anaona akifa mzazi, naye (mtoto) amekwisha?" Kiongozi huyo wa kiroho alihoji.

Alisema malezi maana yake ni kujenga au kupandikiza tabia mpya kwa mtoto na kuitaka jamii inapokuwa inapandikiza mambo hayo, kuzingatia malezi shirikishi na wajibu na kuachana na malezi telekezi na dekezi ya kuwapa watoto kila wanachohitaji kwa kuwa yanasababisha kujenga vijana wasiojiamini na waoga wa maisha.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI**

**Kituo cha DODOMA MJINI**
**Mkoa: DODOMA**

**Shauri la Madai/Ndoa Na 133/2023**

**Jina la Mdai IMARISHA MAISHA FINANCIAL**

**Jina la Mdaiwa ALOYCE R. CHARLES**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa ALOYCE R. CHARLES**
**POLICE CENTRAL**

Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/Waleta madai yake/yao kwamba (Eleza hapa habari za Madai) **TSHS. 1,502,269.71/=**
Hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe **10 Mwezi 07 Mwaka 2023 saa 2:30 asubuhi** kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe **04 Mwezi 05 Mwaka 2023**

A. M. MSANY
PRINCIPAL
PRIMARY COURT MAGISTRATE
URBAN DODOMA

217488802

**THE REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT (CAP.117)**

**CHANGE OF NAME BY DEEDPOLL**

**BY THIS DEED, I VERONICA ELIEZER MGALA** a citizen of Tanzania, **DO HEREBY** wholly , absolutely and utterly renounce, relinquish and abandon the use of my former name of **VERONICA ELIEZER** as it can be seen in my parastatals Pension Fund and adopt as from the date of this deed poll and in substitution of my former name, the name of **VERONICA ELIEZER MGALA** as it appears in my National Identity Card No.19460104-14114-00001-12

For the purpose of evidence of such determination, I, hereby DECLARE that I shall at all times hereinafter in all records, deed, documents and other writings and in all action, suits and proceedings as well as in all Public and Private dealings and transactions and creations whatsoever use and subscribe the said name of **VERONICA ELIEZER MGALA** as my name in lieu and in substitution for my former name **VERONICA ELIEZER**

**AND I HEREBY** expressly authorize and require all and every person and whatsoever at all times after the date hereof to designated, describe and address me by the adopted name of **VERONICA ELIEZER MGALA**

**IN WITNESS WHEREOF** I have set my hand at Dar Es Salaam, and I here on substitute my old of **VERONICA ELIEZER** by my new name of **VERONICA ELIEZER MGALA**

SIGNED and DELIVERED by the said VERONICA ELIEZER MGALA who is known to me personally/identified to me by ........ the latter being known to me personally in my presence this 6th day of JM 2023

DEPONENT



BEFORE:
Signature:
Name: QASSIM MUKED ABDALLAH
Postal address: 35098 DAR-ES-SALAAM
Qualification: ADVOCATE

217488602

# Mganga mbaroni tuhuma kusababisha kifo cha mtoto

**Na Said Hamdani,** LINDI

JESHI la Polisi mkoani Lindi linamshikilia mganga wa kienyeji, mkazi wa Kata ya Rutamba, Manispaa ya Lindi, Jalina Juma (45) kwa tuhuma za kusababisha kifo cha mtoto Yusufu Salum (9).

Mtoto huyo alifariki juzi katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Lindi (Sokoine), alikolazwa kwa ajili ya kupatiwa matibabu kutokana na majeraha ya moto aliyodaiwa kuyapata kwa mganga huyo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, Pilli Mande na Mganga Mfawidhi wa hospitali hiyo, Dk. Alexander Makalla, wamethibitisha kutokea kifo cha mtoto huyo Julai 8 (juzi).

Dk. Makalla alisema mteja wao alifikishwa hospitalini Julai Mosi mwaka huu, akiwa na majeraha makubwa eneo la mgongoni yaliyotokana na kuunguzwa moto.

Alitaja kilichosababisha kifo cha mtoto huyo ni kuenea moto huo ndani ya mwili wake. Ngozi yake ilikuwa haijakomaa.

"Ni kweli mtoto huyo alifikishwa hapa Julai Mosi mwaka huu, akiwa na jeraha kubwa eneo la mgongoni mwake," alisema kiongozi huyo wa hospitali na kubainisha tayari mwili wa mtoto huyo umeshakabidhiwa kwa wazazi wake kwa ajili ya mazishi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, Pilli, alisema mtoto huyo alifikishwa nyumbani kwa mganga huyo na wazazi wake kwa ajili ya kumpatia huduma za matibabu kutokana na ugonjwa wa degedege uliokuwa unamsumbua.

Alidai kuwa baada ya kumfikisha huko, mganga huyo alimpokea na kumlaza juu ya kitanda kisichokuwa na godoro. Uvunguni aliweka nyasi zilizokuwa zinawaka moto na kumuunguza mtoto huyo mgongoni.

Kamanda Pilli alisema wanamshikilia mganga huyo kwa mahojiano ya kina. Wanatarajia kumfikisha mahakamani. Akawataka waganga wa jadi kutumia taaluma zao kwa uangalifu. Waepuke matatizo kama la mganga huyo.

HABARI KITAIFA

# Waziri Mkuu ampa miezi minne DMO ujenzi kituo afya ukamilike

**Na Mwandishi Wetu,**
MTWARA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amemtaka Mganga Mkuu wa Wilaya ya Mtwara, Dk. Matayo Malaika, ahakikishe anasimamia ujenzi wa kituo cha afya Mkunwa ili kikamilike ifikapo Oktoba mwaka huu.

Alitoa agizo hilo juzi alipozungumza na wananchi wa Kata ya Mkunwabaada ya kukagua ujenzi wa kituo hicho kilichoko Halmashauri ya Mtwara Vijijini, mkoani Mtwara. "Nimekagua ujenzi wa kituo hiki cha afya. Nimekuta vifaa vimejaa humo ndani, rangi, masinki ya mikono, vyoo, gutters, marumaru, saruji, vyote vipo na vinakaribia kuharibika.

"Mganga Mkuu simamia huu ujenzi na umshauri vizuri mkurugenzi. Ninataka hatua zote zilizobakia zikamilishwe na hapa ni lazima pawe na watu kwa sababu pana mali za umma.

"DMO mnakaa sana ofisini badala ya eneo la ujenzi. Simamia kituo cha afya hiki kikamilike, una vitu vya afya vitatu na hiki ni cha nne. Milango imekaa tu, jengo lipo, kwanini usiweke hii milango kwenye maeneo yake?" Waziri Mkuu alihoji.

Alimtaka Mhandisi wa Halmashauri hiyo ashirikiane na Mganga Mkuu huyo kuandaa mapitio ya mradi na wapeleke maombi yao Ofisi ya Rais - TAMISEMI ili wapatiwe fedha za kukamilisha majengo ya kituo hicho ambacho alisema kinapaswa kuwa na hadhi ya Hospitali ya Halmashauri kutoka na umuhimu wake kwa eneo hilo. "Kwa sababu hapa pana vyumba vingi, angalieni uwezekano wa kuwa na chumba cha upasuaji cha wagonjwa wa kawaida tofauti na kile kilichoko kule kwenye jengo la kinamama.

"Pia katika mapitio yenu, wekeni wodi tatu ikiwamo ya wanaume, wodi ya wanawake na ya magonjwa mchanganyiko," aliagiza.

Pia aliwataka watendaji hao wakamilishe ujenzi huo kwa sababu tayari serikali ilishatenga Sh. milioni 300 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba vya kituo hicho.

Awali akitoa taarifa ya ujenzi kwa Waziri Mkuu, Dk. Malaika alisema mradi huo ukikamilika utatoa huduma kwa vijiji sita vya Kata ya Mkunwa na kata jirani za Mayanga, Muungano na Dihimba.

Alisema Septemba 2021, halmashauri ilipokea Sh. milioni 250 kwa ajili ya jengo la wagonjwa wa nje (OPD), maabara na kichomeataka.

"Juni 2022, halmashauri ilipokea fedha za awamu ya pili Sh. milioni 250 kwa ajili ya wodi ya wazazi na jengo la upasuaji, njia ya kutembelea na jengo la kufulia yenye hadhi ya kituo cha afya," alisema.

Aliongeza kuwa kutokana na uamuzi wa kuhamishia hospitali ya wilaya kwenda Kata ya Nanguruwe, halmashauri iliomba kibali cha kubadilisha matumizi ili kuendeleza ujenzi wa wodi ya wazazi na jengo la upasuaji vyenye hadhi ya hospitali ya wilaya ambapo ujenzi wake ulianza Novemba, 2022.

"Kwa sasa ujenzi upo hatua ya ukamilishaji na kazi zinazoendelea ni 'skimming', ufungaji wa 'gypsum boards' (dari), uwekaji wa fremu za milango na ujenzi wa marumaru," alisema.

Majengo mengine ambayo yalianza kujengwa na yako katika hatua ya msingi ni ya mionzi, maabara na la kufulia.





**Kampuni ya madini ya Barrick ina lengo endelevu la kuwajengea wadau wake thamani itakayo dumu kwa muda mrefu.** Tunachangia maendeleo ya nchi tulizomo katika nyanja tofauti kupitia shughuli zetu za kijamii na kiuchumi. Sambamba na hilo, tunalinda na kujali usalama na afya ya wafanyakazi wetu. Tunaheshimu na kuthamini haki za binadamu. Aidha, tunafanya shuguli zetu kwa kutunza mazingira na kuzingatia kwamba tunao wajibu wa kuacha urithi wa maliasili kwa ajili ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo pia.








TWIGA Minerals Corporation Limited

NYSE : GOLD • TSX : ABX
www.barrick.com

dP 6595
217488302


## Songwe yatajwa kuathirika biashara haramu utumikishwaji wa binadamu

**Na Ibrahim Yassin,**
SONGWE

KUELEKEA maadhimisho ya kupinga usafirishaji haramu wa binadamu duniani Julai 30, mwaka huu, Mkoa wa Songwe umetajwa watu wake kuathirika na biashara hiyo kwa kusafirishwa nchi za nje kutumikishwa.

Akifungua mafunzo mwishoni mwa wiki, Katibu wa Sekretarieti ya Kuzuia na Kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Separatus Fella, alisema mafunzo hayo yanayotolewa na Shirika la Tanzania Relief Initiatives (TRI) na kufadhiliwa na Hanna Seidlel Foundation maalumu kwa ajili ya kuwajengea uwezo wadau mbalimbali mkoani humo wanaotekeleza sheria inayozuia usafirishaji haramu wa binadamu ambayo Mkoa wa Songwe yanafanyika kwa mara ya kwanza.

"Katika utendaji wetu wa kazi imekuja kuonekana Songwe ni sehemu ambayo watu wanasafirishwa kwenda sehemu mbalimbali na wanavushwa mpaka nje ya nchi, wengine wanapelekwa Kenya na nchi zingine kwenda kutumikishwa," alisema Fella.

Alisema kuwa hali ya mapambano kwa serikali inajitahidi kwa kushirikisha wadau mbalimbali wakiwamo IOM, IWOB, UNODC, KIWOHEDE, SALVATION, ROME CENTER na kutumia mafunzo kama hayo katika kusaidia kupambana na biashara hiyo pamoja na kufanya mabadiliko ya sheria ambazo zinasaidia katika mapambano ya biashara hiyo.

Aidha, Mkurugenzi wa miradi kutoka TRI, Damiani Edward, alisema mafunzo hayo yamejikita kuwajengea uwezo wadau mahsusi wanaojikita katika kusimamia sheria mbalimbali ikiwamo inayopinga usafirishaji haramu wa binadamu, wadau walioshiriki mafunzo hayo ni pamoja na Jeshi la Polisi, maofisa Uhamiaji, mahakama, kazi, ustawi wa jamii na waendesha mashtaka.

Alisema zaidi ya kesi 72 za usafirishaji haramu wa binadamu zimefunguliwa na wahalifu 123 wamehukumiwa, waathirika 892 waliokolewa na kusaidiwa na mafunzo yamefanyika mikoa 19 Tanzania Bara na Visiwani na tayari watekelezaji 2000 wa sheria wamepatiwa mafunzo.

"Wahanga wakubwa wa biashara haramu ni wanawake, vijana na watoto ambao hudanganywa kwa kuahidiwa kazi nzuri ikiwamo kuuza maduka mijini katika miji mikubwa kama Dar es Salaam, Mwanza na Arusha au nje ya nchi na badala yake hujikuta wakipelekwa kutumikishwa," alisema Edward.

# Ndege mpya ya mizigo ATCL yaanza safari

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Ndege Air Tanzania (ATCL) imeanza safari yake ya kwanza juzi ya ratiba ya kusafirisha mizigo kwa kutumia ndege yake ya mizigo Boeing 767-300F iliyowasili nchini mapema mwezi Juni 2023.

Mkurugenzi wa Biashara wa Kampuni hiyo, Patrick Ndekena, alitoa taarifa hiyo mwishoni mwa wiki wakati akiongea na waandishi wa habari, katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam.

Alisema ratiba ya safari za Dubai itakuwa mara mbili kwa wiki na jukumu la ATCL kwa ndege hiyo ni kuhakikisha bidhaa za wafanyabiashara wa ndani na nje ya nchi zinafika kwa wakati na zikiwa na ubora wake kwenye nchi mbalimbali kwa kadri ya mahitaji.

"Leo (juzi) tunafuraha kubwa kwa kuanza rasmi safari zetu za ratiba kwa ndege yetu hii mpya ya mizigo Boeing 767-300F yenye uwezo wa kusafiri masafa marefu na uzito mkubwa yaani tani 54 kwa mara moja, kwa Dubai peke yake tutakuwa na safari mbili kwa wiki, Jumatatu na Ijumaa."

Akifafanua kuhusu uwezo wa ndege hiyo, alisema Boeing 767-300F ni ndege ya kisasa yenye uwezo wa kusafiri umbali wa kilomita 850 kwa saa na kukaa angani kwa zaidi ya saa 10 bila kutua.

Kuhusu wataalamu wa ndege hiyo alisema kuwa ATCL ina marubani wakitanzania sita waliobobea kwenye ndege hiyo. Wataalamu wengine wabobezi ni pamoja na wahandisi wa ndege ambao pia ni Watanzania.

Ndekana amemshukuru Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuiwezesha ATCL kujiendesha kibiashara. Naye wakala wa usafirishaji mizigo, George Magoti, amesema kuwapo kwa ndege hiyo ni mkombozi kwa wafanyabiashara nchini kwa kuwa itawasaidia kupunguza gharama za usafirishaji.

Alifafanua kutokana na ukubwa wa mizigo hiyo, isingewezekana kusafirishwa kwa ndege ya abiria na wangelazimika kukodi ndege ya mizigo kutoka nje ya Tanzania ili kupakia mizigo mikubwa ya aina hiyo.

"Tunashukuru ATCL kukubali kufanyabiashara nasi ya mizigo la sivyo tungelazimika kutafuta ndege kutoka nchi zingine ambapo ingeongeza gharama, kuchelewesha muda kusubiri ndege ifike na usumbufu wa vibali vya hiyo ndege ya nje," alisema Magoti.

Pia, alisema mzigo uliopakiwa na Air Tanzania utapelekwa hadi Dubai na kutoka hapo utasafirishwa kwenda Marekani kwa urahisi na uharaka kuliko wangetumia usafiri mwingine.

Mpango wa ununuzi wa ndege ya mizigo umelenga kurahisisha usafirishaji wa bidhaa kutoka na kuingia Tanzania na hivyo kuongeza thamani ya bidhaa nchini.




Ndege mpya ya mizigo ikiwa inapakia mizigo tayari kwa safari. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali kusaidia mradi wa satelaiti

**Na Mary Geofrey**

SERIKALI imeahidi kusaidia mradi wa Nano Satelaiti uliobuniwa na wahadhiri na wanafunzi wa Idara ya Sayansi ya Kompyuta na Mfumo wa Habari wa Chuo Kikuu cha Mt. Joseph (SJUIT), ambao utazindua satelaiti ya kwanza ya juu nchini.

Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mathew Kundo, alitoa ahadi hiyo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam katika maonyesho ya tatu ya sayansi na teknolojia ya chuo hicho.

Alisema maonyesho hayo yanaonyesha utayari wa wasomi kushiriki katika soko la ajira wakiamini kuwa kwa maarifa mapya na msaada kutoka kwa serikali na wadau, utaongeza kasi ya nchi kusonga mbele katika utafiti na uwekezaji wa viwanda.

"Bila shaka mnasoma katika zama ambazo kuna nafasi kubwa ya uvumbuzi unaolenga kuleta suluhisho kwa jamii.

"Ninapenda kuwahakikishia kuwa serikali itawapa ushirikiano wa hali ya juu ili kusaidia safari mliyoanza kwa uvumbuzi wa satelaiti.

"Maonesho haya yamethibitisha kuwa elimu inayotolewa Tanzania hasa SJUIT ina ubora wa hali ya juu. Inathibitisha kwamba wanafunzi wetu hawana tofauti na wale walio nje ya nchi," alipongeza.

Naibu Waziri huyo pia aliipongeza SJUIT kwa kutekeleza kwa vitendo maelekezo ya hivi karibuni yaliyotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan, kuanzisha mchakato wa uvumbuzi wa satelaiti.

Rais wa Baraza la SJUIT, Dk. Thomson Ananth, alisema chuo hicho kilianzisha mradi huo mwaka 2020, kupitia Kituo cha Uvumbuzi na Teknolojia (ITAF) ili kutimiza maono ya serikali katika kutengeneza nafasi kwa kuzindua satelaiti ya kwanza nchini.

"Tumeshirikiana na taasisi za mafunzo kutoka India kufundisha wanafunzi wetu 30 na wahadhiri watano ambao wanafanya kazi katika mradi huu.

"Hii inafanywa hasa kwa kuwajengea uwezo Watanzania ili kutimiza dira ya serikali katika kuzindua anga yake ya satelaiti.

"Katika mwaka huu wa masomo wa 2022/23, miezi michache ijayo tunatarajia satellite yetu ya Nano kuanza kuingia katika mzunguko kwa kutumia roketi ya gari la uzinduzi kutoka India," alisema.

Mjumbe wa Baraza la SJUIT, Gertrude Mongella, alisema kipengele cha wanawake katika teknolojia kinaonesha jinsi wanawake wanavyoachwa nyuma kutokana na sababu mbalimbali.

Alisema takwimu za hivi karibuni zinaonesha namna wanawake wanavyopiga hatua moja mbele kushikilia nafasi sawa na wanaume katika sekta ya uvumbuzi.

## Botswana waja kujifunza utunzaji vyanzo vya maji

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SERIKALI ya Botswana imewataka Watanzania kuendelea kutunza kwa gharama yoyote vyanzo vya maji na rasilimali zake kwakuwa maji ndiyo yanachangia maisha ya binadamu na yakikosekana yataathiri mfumo mzima wa maisha.

Kauli hiyo ya Serikali ya Botswana imetolewa na Mhandisi wa Maji kutoka Kitengo cha Kuhudumia Idara ya Maji na Usafi wa Mazingira, Saniso Sukuringwa, wakati alipotembelea mradi wa jengo la Jumuiya ya Watumia Maji Mvuha chini na utunzaji wa vyanzo vya maji iliyopo Kijiji cha Lukulunge, halmashauri ya Wilaya ya Morogoro, mkoani humo kwa lengo la kujifunza kutunza vyanzo vya maji.

Mhandisi Sukuringwa alisema, anaionea wivu Tanzania kuwa na vyanzo vingi vya maji pamoja na milima na misitu iliyohifadhiwa vizuri na kuwataka Watanzania kamwe wasikubali vyanzo hivyo vipotee.

Alisema nchi yao kwa sasa inalazimika kutoa maji nje ya nchi kwaajili ya matumizi ya ndani kutokana na sehemu kubwa kuwa na jangwa na kukosekana kwa milima pamoja na maeneo ya hifadhi ya misitu.

"Nimekuja Tanzania nimeona mna milima mingi sana, misitu iliyofungana na vyanzo vya maji mengine yanamwagika yenyewe tu, ninawaonea wivu sana kwakuwa kule kwetu kuna jangwa hivyo hakikisheni mnatunza vyanzo vya maji na kuhifadhi mazingira kwa gharama yoyote kwakuwa hakuna mbadala wa maji na maji ndiyo kila kitu," alisema Sukuringwa.

Naye Mhandisi Irene Madilola kutoka Botswana, aliishukuru Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Maji kutoa nafasi ya wao kujifunza na kupeleka mbinu za utunzaji wa mazingira na vyanzo vya maji katika nchi yao huku wakihaidi kurudi tena.

Mhandisi Madilola aliwataka watanzania kwenda nchini Botswana kwaajili ya kujifunza au kujionea jangwa lilopo nchini humo na kulazimika kutoa maji kutoka nje ya nchini.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Globol Water Patnership, ambao wamefadhili ujenzi wa jengo hilo la Jumuiya ya Watumia maji wa Mvuha chini, alisema umegharimu jumla ya Sh. milioni 75 zilizotolewa na Jumuiya ya Ulaya.

Alisema wafadhili wa mradi huo pia wamefadhili mradi kama huo nchini Botswana huku akiishukuru Serikali ya Tanzania kuwa na mahusiano mazuri na Jumuiya na wadau wa ndani na nje wanaotunza rasilimali za maji na usafi wa mazingira.

Naye Mhandisi Kalunde Malale, akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi wa Rasilimali za maji kutoka Wizara ya Maji, alisema serikali itaendelea kushirikisha wananchi kwaajili ya utunzaji wa vyanzo vya maji nchini ili viendelee kuwapo.

Awali, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Watumiaji Maji Mvuha chini, Mussa Mgamba, alisema changamoto iliyopo kwao ni wafugaji kunyweshea mifugo yao kwenye vyanzo vya maji na kuiomba serikali na wadau wengine kuwajengea birika wafugaji hao kwaajili ya mifugo ili vyanzo hivyo viendelee kuhifadhiwa.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Waamuzi wapigwe msasa zaidi tuone thamani ya usajili Ligi Kuu

**KLABU** za Ligi Kuu, Championship, First League na Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania Bara, kwa sasa zipo katika hekaheka kubwa ya kuendelea kufanya usajili, tangu dirisha hilo lilipofunguliwa rasmi Julai Mosi, mwaka huu.

Tayari klabu kadhaa hususan za Ligi Kuu zimetangaza wachezaji wao wapya waliokwamisha usajili, huku baadhi zikitangaza kukamilisha usajili kabla hata ya dirisha hilo kufungwa Agosti 31, mwaka huu.

Kwa ujumla klabu zinatumia gharama kubwa kufanya usajili hasa kwa wachezaji wakigeni, ambao mbali na fedha za usajili na mishahara zitakazowalipa bado wanalipiwa vibali vya kufanya kazi nchini na mambo mengi mengi.

Hivyo, matarajio ya klabu husika ni kuona zinafaidika kwa kuziwezesha kupata matokeo chanya na mwisho wa msimu kukamilisha malengo waliyojiwekea kabla ya wa msimu kuanza, hususan kutwaa mataji.

Hata hivyo, kwa misimu kadhaa tumeshuhudia baadhi ya waamuzi wakipeperusha malengo hayo ya klabu kutokana na kushindwa kuchezesha mpira kwa kufuata sheria 17 za soka duniani, ama kufanya makusudi kwa dhamira zao wenyewe.

Hivyo, wakati huu klabu zikiendelea kufanya usajili pamoja na maandalizi ya msimu mpya, tunatamani kuona Shirikisho la Soka nchini (TFF), pamoja na Bodi ya Ligi (TPLB), zikishirikiana na Chama cha Waamuzi nchini (FRAT), kuwaandaa waamuzi kwa kuwapiga msasa zaidi hususan kuwakumbusha sheria za soka na mabadiliko mbalimbali ya kanuni.

Kwa kufanya hivyo, tunaamini msimu mpya wa Ligi 2023/24 utakapoanza, kutasaidi kupunguza ama kuondoka makosa kabisa ambayo mara kadhaa yamekuwa yakielezwa ni ya 'kibinadamu'.

Tunataka kuona ligi yetu ikizidi kupanda viwango na kuwa kati ya Ligi Kuu bora tatu barani Afrika na hilo haliwezi kutokea kwa klabu kusajili wachezaji bora pekee, bali pia kwa kuwa na waamuzi bora wanaotenda haki kwa kufuata sheria 17 za soka huku miundombinu ya viwanja ikiboreshwa zaidi.

Lakini pia tunataka kuona klabu zikifanikiwa kutimiza malengo yao na kuona faida ya gharama kubwa walizotumia katika dirisha hili la usajili.

Pamoja na hayo yote, pia umefika wakati wa waamuzi wenyewe kutumia kipindi hiki kwa kujifunza wenyewe kanuni mbalimbali zilizofanyiwa marekebisho ili watakapopewa jukumu la kusimamia mechi kuhakikisha wanatenda haki kwa kila timu.


Sisi tunaamini kama hilo likifanyika, ushindani katika ligi yetu utaongezeka na kuvutia wachezaji wakubwa zaidi kuja kucheza soka nchini, lakini likiwa ni suluhisho kwa kilio cha muda mrefu cha TFF kuhusu mashabiki wengi kwenda viwanjani.

Aidha, tunaitaka pia TPLB kuandaa ratiba rafiki kwa kila klabu ili kuwezesha kuwa na ushindani wa kweli na si kuona baadhi ya timu zikicheza mechi hadi tatu mfululizo nyumbani ama ugenini kama ilivyokuwa kwa msimu uliomalizika.

Nipashe tunazitakia timu zote za Ligi Kuu za wanaume na wanawake, Championship na First League maandalizi mema kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu 2023/24, kwani matarajio yetu ni msimu ujao ni kuona ushindani ukiongezeka zaidi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Klabu malizeni usajili kabla ya 'pre season'

Na Adam Fungamwango

**KLABU** nchini zimeanza kujipanga kwa maandalizi ya msimu ujao wa mashindano ya kitaifa na kimataifa.

Mabingwa Watetezi, Yanga kwa mujibu wa Meneja wake, Walter Harisson, watapiga kambi nchini na wachezaji wake wataanza kuwasili leo kabla ya kuanza 'pre season.'

Meneja Habari wa Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, yeye amebainisha kuwa kikosi cha Simba kinatarajia kuondoka kesho kwenda nchini Uturuki kuweka kambi, huku Azam FC yenyewe ilitarajiwa kuondoka jana kwenda nchini Tunisia kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya.

Singida Fountaine Gate itakuwa jijini Arusha kuweka kambi yake huko kwa mujibu wa msemaji wake, Hussein Massanza.

Prisons, kwa mujibu wa msemaji wake, Jackson Mwafulango, itafanya 'pre season' yake kwenye moja kati ya mikoa minne, nayo ni, Musoma mkoani Mara, Mwanza, Zanzibar au Dar es Salaam.

Hizo ni zile timu ambazo tayari zimeweka wazi mipango yao ya maandalizi, zipo ambazo hazijafanya hivyo, lakini zipo kwenye maandalizi kabambe.

Ni kipindi ambacho makocha hukitumia kuanza kuwaweka wachezaji kwenye utayari wa kimwili na kiakili kuanza kuzitumikia kwa msimu ujao.

Makocha na benchi la ufundi hutumia kiasi cha wiki moja na nusu au mbili kuwaweka kwenye utimamu wa mwili na baada ya hapo ndipo huanza kuwaweka chini wachezaji kuwaeleza mbinu zake, mifumo na baadaye kuifanyia kazi uwanjani.

Ni kipindi muhimu ambacho hakitakiwi kufanyiwa masihara hata chembe kwa sababu mchezaji yeyote hata akiwa mzuri kiasi gani kama hakupata 'pre season' nzuri iliyoshiba, hawezi kuwa na kiwango kizuri kwa msimu mzima.

Kibaya zaidi inawezekana kabisa mchezaji huyo pia akawa anaumia mara kwa mara kwa sababu mwili wake hauko timamu. Wachezaji wanaokosa mazoezi hayo wana tabia pia ya kuchoka haraka.

Kwa bahati mbaya sana kuna tatizo dogo la uelewa au uwezo kwenye klabu nyingi za Tanzania ambazo zinasajili wakati wachezaji wapo kwenye 'pre season.'

Zipo zingine labda kwa sababu za kiuchumi na ufinyu wa ratiba zinaanza maandalizi ya msimu mpya na wachezaji wengine, huku zikiwa hazijasajili hata mchezaji mmoja, halafu wakati kambi ikiendelea ndiyo zinaanza kusajili mmoja mmoja kwa kasi ya kobe, matokeo yake wanaokuja wapya hawaleti kile kitu kilichokusudiwa ndani ya timu kwa sababu hawana utimamu wa mwili, hawakufanya 'pre season' sawa sawa.

Hiki ndicho kilichoikumba Simba misimu miwili iliyopita. Ilikuwa ikifanya 'pre seaon' nje ya nchi ikiwa haina wachezaji wapya, na walikuwa wakisajiliwa ikiwa inakaribia kumalizika, au imeshaisha kabisa. Matokeo yake kila mtu ameyaona.

Naona msimu huu imegundua kosa lake, imesajili mapema, ingawa inasema haijamaliza, lakini kwa kiasi kikubwa imeweza kurekebisha makosa yake.

Hata kama kuna ukata, lakini klabu zote zinazocheza Ligi Kuu na Ligi ya Championship zizingatie jambo hili, kuepuka tabia ya kufanya maandalizi zikiwa ndiyo zinaanza kusajili.

Ninachoshukuru ni kwamba baadhi ya klabu zimeanza kuelewa jambo hili.

"Safari hii kuelekea msimu ujao tunataka kufanya 'pre season' ya nguvu, viongozi wa juu wamesema maandalizi yaanze mapema na tuchague sehemu ya kufanya maandalizi hayo tukiwa na wachezaji wote wapya," alisema Mwafulango wa Prisons.

Ili kuleta ushindani wa kweli kwenye Ligi Kuu hasa kwa timu zinazoitwa au kujiita ndogo, zimalize usajili na ziende 'pre season' zikiwa na wachezaji wote wa zamani na wapya, zitakuja kunishukuru baadaye.

# Kesi wabunge 19 CHADEMA kupinga kuvuliwa uanachama kuendelea leo

**Na Grace Gurisha**

KESI ya kupinga kuvuliwa uanachama iliyofunguliwa na wabunge 19 wa Viti Maalum kupitia Chama cha Demokrasia (CHADEMA), inaendelea kusikilizwa leo katika Mahakama Kuu Masjala Kuu, Dar es Salaam huku mjumbe wa Bodi ya Wadhamini wa chama hicho, Lucy Mollel, anatarajiwa kuulizwa maswali ya dodoso na mawakili wa wabunge hao.

Maswali hayo ataulizwa mbele ya Jaji Cyprian Mkeha, kutokana na kiapo kinzani alichokiwasilisha mahakamani hapo, baada ya Mbunge wa Viti Maalum, Halima Mdee na wenzake 18 kufungua kesi kupinga kuvuliwa uanachama na chama hicho.

Machi 6, 2023 Wakili wa wajibu maombi, Ipilinga Panya, aliiomba mahakama itoe hati za wito za wajumbe saba wa bodi hiyo ili waje mahakamani kujibu maswali ya dodoso kuhusiana na viapo vyao kinzani katika maombi hayo.

Panya, aliwataja wajumbe hao kuwa ni Profesa Azaveri Lwaitama, Silvester Masinde, Lucy Mollel, Mary Joakim, Francis Mushi, Maulida Komu na Ahmed Hamis.

Hadi sasa aliyeulizwa maswali ya dodoso ni Profesa Lwaitama, ambaye alidai kuwa Mdee na wenzake hata kama walipata matishio ya usalama wao kuwa kuna watu wataandamana, "tufikirie tu enzi za Rais Dk. John Magufuli kuna mtu anaweza kufanya maandamano au ilikuwa janja janja yao tu."

Mbali Panya mawakili wengine ni Aliko Mwamanenge, Edson Kilatu, Emmanuel Ukashu, Joyce Mwakakila na Afrey Maunga, upande wa wajibu maombi yupo Wakili Peter Kibatala na Jeremiah Mtobesya.

Mdee na wenzake walifungua shauri hilo namba 36/2022 Julai 22, 2022 wakiomba mahakama hiyo ipitie mchakato na uamuzi wa kuwafukuza uanachama na kisha itoe amri tatu.

Katika shauri hilo, wabunge hao wanaiomba mahakama itengue mchakato na uamuzi wa kuwavua uanachama na pia iwalazimishe Chadema kuwapa haki ya kuwasikiliza.

Pia, wanaomba amri ya zuio dhidi ya Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), kutokuchukua hatua yoyote hadi malalamiko yao yatakapotolewa uamuzi.

# 'Tembo Nickel kubadilisha sekta ya madini'

**Na Mwandishi Wetu,**
NGARA

KAMISHNA wa Madini kutoka Tume ya Madini, Janet Lekashingo, ametembelea Mradi wa Kabanga Nickel wilayani Ngara, Mkoa wa Kagera na kusema mradi huo utaleta mabadiliko makubwa kwenye sekta ya madini nchini.

Lekashingo aliambatana na Ofisa Madini Mkazi wa Kagera (RMO), Samwel Shoo, Mjiolojia kutoka Tume ya Madini Dodoma, Innocent Mabiba na Mwanasayansi wa Mazingira kutoka Ofisi ya RMO Kagera, Benedict Sekihaba.

"Mradi wa Kabanga Nickel unaoendeshwa na kampuni ya Tembo Nickel ni mradi muhimu sana kwetu, tunaenda kwenye madini ya kimkakati, hii ni moja ya game changer kwa Tanzania (inabadilisha mchezo kwa Tanzania). Si kwa sababu ni madini ya kimkakati ila ni kwasababu itatengeneza madini haya mpaka zao la mwisho hapa nchini. Kwa hiyo nyie ni wadau na wawekezaji wa muhimu kwetu sisi na tunaliheshimu hilo," alisema.

Alisema Tembo Nickel kuwa na ubia na Lifezone, BHP na Serikali ya Tanzania, ni jambo linaloonyesha kuwa kampuni hiyo italeta matumaini kwa taifa.

Lekashingo pia alipongeza hatua ya Tembo Nickel kufanya utafiti wa ujuzi ili kujua aina ya ujuzi ulio wilayani Ngara na kusema kuwa kufanya kazi na jamii inayozunguka mradi ni siri ya mafanikio.

"Mkitaka kukaa vizuri, hamwibiwi vitu inatakiwa wananchi wawalinde, nimefurahi kuwa mmefanya utafiti wa ujuzi, kwa hiyo mnajua mna watu wa aina gani," alisema.

Aliipongeza Tembo Nickel kwa kuanza programu maalumu ya kuchukua wahitimu wa vyuo vikuu kwenye fani mbalimbali na kuwapa kazi ili wajifunze kwa vitendo.

"Nina furaha kwamba mmefanya mpango wa wahitimu wa vyuo vikuu, hakuna kitu kizuri kama mpango wa wahitimu wa vyuo," alisema.

Pia alisema mpango huo ni mzuri kwa kuwa unaendelea kutengeneza nguvu kazi kwa taifa.

"Mtu akifanya kazi mgodini na anafanya kile alichosomea hata kwa mwaka mmoja akitoka ataenda kuwa mkandarasi wenu, ama ataenda kufanya kitu huko Tanzania, hili ni eneo la kujifunza ambalo ni nzuri sana," alisema.

Alisema pia Tembo Nickel ni mgodi unaoanza baada ya miaka 20 tangu kuanze kuwa na migodi mikubwa nchini, alitaka uzoefu uliopatikana katika kipindi hicho utumike kuhakikisha mradi huo unakuwa wa mfano.

Naye Meneja wa Usalama na Afya Mahala pa Kazi, Dk. Kudra Said, alisema Tembo Nickel imeshafanya utafiti wa ujuzi kwa awamu mbili katika Wilaya ya Ngara ili kupata watu wa kufanya kazi kwenye mradi.

Alisema pia, katika mpango wa wahitimu wa vyuo, waombaji waliojitokeza walikuwa 7,143 na waliokuwa wanatakiwa ni 12 pekee.


## Bank of India (Tanzania) Ltd.

*Relationships beyond banking*

**Fully owned subsidiary of Bank of India (Public Sector Bank)**

ISCLOSURES MADE UNDER REGULATION 11 OF BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS (DISCLOSURES) REGULATIONS, 2014 AND CONSUMER PROTECTION REGULATION, 2019

## MINIMUM DISCLOSURE OF CHARGES AND FEES (GHARAMA ZA HUDUMA ZETU)

**Service Charges (Exclusive of VAT and Government Levy on DigitalTransactions)**
**(The applicable VAT (Value added Tax) and Govt Levy on digital Transaction to be collected during the collection of service charges)**

### A. REMITTANCE -OUTWARD

| Sr. No. | Item | Charge |
|---|---|---|
| **TISS Remittance** (Only for A/c holders – Not permitted for non a/c holders) | Remittance -TZS | TZS 10,000 |
| | Remittance -USD | USD 10 |
| **Other Outward Remittance** | 1USD up to 6,000 | USD 15 |
| | USD 6,001 – 10,000 | USD 30 |
| | Above USD10,000 | @ 0.35% Maximum USD 75 |
| Tracer Charges | Irrespective of Amount | USD 30 |
| Recall back funds charges | Irrespective of Amount | USD 30 |

### B. REMITTANCE -INWARD

| Sr. No. | Item | Charge |
|---|---|---|
| (Only for A/c holders – Not permitted for non a/c holders) | From inside Tanzania | Free |
| | From outside Tanzania: as under | |
| | For Current /Overdraft Accounts | 0.35% of inwards remittance Minimum USD 18 Maximum USD 70. |
| | For Saving Accounts | |
| | USD 0 up to USD 100 | Free |
| | USD 101 up to USD 500 | USD 10 |
| | Above USD 500 | USD 18 |

### C. DEPOSIT AND RELATED SERVICES

| Item | TZS A/c | USD A/c |
|---|---|---|
| **Saving Account :-** | | |
| Cash withdrawal per day -Free of charge, up to amount | TZS 25 Mn | USD 2000 |
| Cash withdrawal charges over USD 2,000 to USD 5000 per day | – | 0.25% of withdraw amount |
| Cash withdrawal charges over USD 5,000 per day | – | 0.60% of withdraw amount |
| Cash withdrawal charges over TZS 25 Mn per day | 0.10% of withdrawal amount | |
| Cash Deposit charges over USD 5,000 per day | – | 0.60% of deposited amount |
| Cash deposit charges for small currency USD notes ranging from USD 1 to USD 20, irrespective of amount deposited (i.e. both for below and above USD 5,000) | – | 12% (Min USD 1) of the aggregate small currency amount |
| **Current Account:-** | | |
| Cash withdrawal per day -Free of charge, up to amount | TZS 25 Mn | USD 5000 |
| Cash withdrawal charges over USD 5,000 per day | – | 0.60% of withdrawal amount |
| Cash withdrawal charges over TZS 25.00 Mn per day | 0.15% of withdrawal amount | – |
| Cash deposit charges over USD 10,000 per day | | 0.60% of deposit |
| **Maintenance of minimum balance: -** | | |
| For Saving Account-Without Cheque Book Facility | TZS 50,000 | USD 50 |
| With Cheque Book Facility | TZS 200,000 | USD 200 |
| For Current Account | TZS 200,000 | USD 200 |
| **Minimum balance charges (in case of non-maintenance of minimum balance)** | | |
| Saving Account - Without cheque book | TZS 900 p.m | USD 4 p.m |
| With cheque book | TZS 3600 pm | USD 15 p.m |
| Current Account- | TZS 20,000 p.m | USD 15 p.m |

### D. Other Common Charges

| Item | Charges TZS A/c | Charges USD A/c |
|---|---|---|
| Stop Payment Instructions | TZS 35,000 | USD 28 |
| Regular statement of a/c (Monthly) | Free | Free |
| Interim/additional statement | TZS 1500 per page | USD 1.50 per page |
| Issue of bankers' cheque | TZS 40,000 | USD 30 |
| Cancellation of bankers cheque/DD | TZS 20,000 | USD 15 |
| Issue of Duplicate Bankers cheque/Demand Draft/ Duplicate FDR | TZS 30,000 | USD 20 |
| Application charge for Treasury Bond | TZS 100,000 | USD Equivalent to TZS 100,000 |
| Issue of Balance certificate (Saving Account) | TZS 20,000 | USD Equivalent to TZS 20,000 |
| Issue of Balance certificate (Current Account) | TZS 50,000 | USD Equivalent to TZS 50,000 |
| Signature verification and Photo Attestation charges for Domestic A/c Holders | TZS 10,000 | USD Equivalent to TZS 10,000 |
| Verification of Documents such as KYC Documents along with verification of Photo and Signature of Customer Mentioned account with Bank of India- in India /Overseas | TZS 25,000 | USD Equivalent to TZS 25,000 |
| Savings bank customer Identification card- One time | TZS 20,000 | USD 10 |
| Dormant a/c Activation Per Activation Fees | Individual TZS 5,000 Corporate TZS 12,000 | Individual USD 3 Corporate USD 6 |
| Account Freezing/un freezing Charges | Free | Free |
| SMS Alert facility | Free | Free |
| Email Alert Facility | Free | Free |
| Monthly Statement on Registered Email | Free | Free |
| Balance Inquiry (Over the Counter) | Free | Free |
| Charges for Deletion of Decease Person Name from the Saving Account | Free | Free |
| Charges for Addition/modification Account such as Change in respect of Corporate A/c | TZS 20,000 | USD 10 |
| Updating of Mobile No. in A/c (SB,CD,OD) | Free | Free |
| Change /Modification in Address (SB,CD,OD) | Free | Free |
| Issuance of No Dues Certificate for Non-Borrowers. | TZS 10,000 | USD 7 |
| Ledger Folio Charges per Folio (40 lines per Folio) only for Current and Overdraft Accounts | TZS 6,000 per Folio | USD 4 per Folio |
| Postages/Courier Charges Inland/Foreign | TZS 30,000 or actual charges whichever is higher | USD Equivalent to TZS 30,000 |

### E. CLEARING SERVICES

| Item | Charge/Fees TZS A/c | Charge/Fees USD A/c |
|---|---|---|
| Within walking distance-1 km | TZS 70,000 | USD 45 |
| Far off distance -more than 1 km | TZS 95,000 | USD 65 |
| Cheque returned charges -financial reasons (inward/outward) | TZS 70,000 | USD 55 |
| Inward/outward cheque collection - USD | 0.60% Min comm.18 postages 90 | 0.60% Min comm.18 postages 90 |

### CREDIT MATTERS

| Item | Charge/Fees | |
|---|---|---|
| **Proposal Processing Charges: -** | | |
| New Overdraft/Term Loan/Demand Loan | 1.50% of sanctioned limit (Regular Limit – 1.50% for 12 Months) | |
| TOD/TOL/ADHOC | Proportionate to 1.50% for TOL/TOD/ADHOC Period minimum USD 60 | |
| New NFB BG/LC Facility | 1.50% of sanctioned limit (Regular Limit – 1.50% for 12 Months) | |
| Review of Overdraft Limit | 1.50% on entire sanctioned amount. | |
| Review of Term Loan Demand Loan Personal Loan Vehicle Loan Loan Against Property Etc. | 0.15% maximum USD 600 or TZS 1.20Mn on the reviewed amount and 1.50% on the additional Term Loan /Demand Loan amount. | |
| Schematic Lending up to 36 months/Staff Loan | Nil | |
| Prepayment charges | 2.50% of the prepaid loan amount. | |
| Documentation charges for New Overdraft Limit/Term Loan/Demand Loan/Non Fund base Limit | Actuals as per advocate Bill + 0.30% handling charges<br>1. No Documents charges would be applicable for TOD/TOL/ADHOC Limit, however actual expenses if any to be recovered.<br>2. Documentation charges also NOT Recoverable for the Loan/Overdraft against FDR. | |
| Charges for Amendments/Modification of Sanction Terms | 0.25% on the sanctioned limit<br>**We enumerate the illustrative instances of Modification in Terms and Conditions to be effected at the request of the Borrower where this charge will be levied: -**<br>1. Substitution of Collateral Securities/Personal Guarantee<br>2. Release of Personal Guarantee/Collateral Security.<br>3. Interchangeability of limits.<br>4. Change in project/items of Machinery<br>5. Ceding of charges on assets(Pari-Passu)<br>6. Restructuring, Rephasement of Loans/ Deferment of Loan installments.<br>7. Approvals for mergers & amalgamations.<br>8. Any other miscellaneous credit related approvals. | |
| Revalidation of Sanction | **25% of Applicable PPC Charges on Overdraft Limit/Term Loan/Demand Loan** | |
| Lead bank Charges | **USD 1000 or equivalent in TZS per annum/one time** | |
| Fee for Opening Escrow/TRA A/cs (Trust and Retention A/cs) | **Where**<br>**We are Lead bank: Nil**<br>**We are Not Lead Bank:**<br>USD 500 or equivalent in TZS per annum/one time | |
| Charges for Supplying copies of Loaning Documents to Customer. | First instance: Free<br>**USD 10 or equivalent in TZS for further requirement.** | |
| Non/Delayed Submission of Audited Financial Statements of the Company OR wherever applicable | **USD 100 or equivalent in TZS per month or part thereof**<br>**Note:-**Audited Financial statements of the firm/company within 6 months from closure of Financial Year or as approved by TRA for the relevant year. | |
| Inspection charge | TZS 30,000 per visit/inspection or at least once in quarter whichever is higher. | TZS 50,000 or equivalent to USD per visit /inspection or at least once in quarter whichever is higher. |
| | **Note:-**<br>1. Out of Pocket Expenses to be recovered additionally along with regular inspection charges wherever applicable<br>2. **Project Monitoring Inspection Charges/Technical Due Diligence Inspection charges:** Considering the fact that this inspection is proposed for safeguarding banks Interest, normal inspection charges besides travelling, boarding/lodging expenses are to be recovered from the borrower. | |
| Issuance of No objection certificate (NOC) | **USD 100 or equivalent in TZS** | |
| 1st party/3rd party Overdraft/Loan against deposit of our Bank (BOITL) | Waiver of Processing & Documentation charge. | |
| Overdraft/Term Loan/Demand Loan Conversion Charges (Currency Conversion) | For Overdraft account 0.50% of Sanction Limit.<br>For Term Loan/Demand Loan 0.50% of O/s Amount | |
| Earmarking of Limits | **USD 500 or equivalent in TZS per annum** | |
| Non Compliance of Sanction terms/Commitment charges | **1.00% additional Penal Interest to be charge till compliance of Sanction terms** | |

| D&B/ Other Credit Information Search for per Borrowal a/c (New/Additional/Review of limit) | USD Facility | TZS Facility |
|---|---|---|
| Up to TZS 20 Mn/USD 10,000 (Only for new and additional Limit. **Review – No charge**) | USD 5 | TZS 5,000 |
| Over USD 10,000 to USD 50,000/ Over TZS 20 Mn up to TZS 100 Mn | USD 10 | TZS 20,000 |
| Over USD 50,000/TZS 100 Mn | USD 50 | TZS 100,000 |
| D&B Search for non-Borrower, on request | USD 50 | TZS 100,000 |
| Charges for Furnishing copy of Credit Information report obtained from CIC | TZS 20,000 | USD 10 |

| Item | Charge | |
|---|---|---|
| **Guarantee (Performance/Financial) :-** | | |
| Guarantee Commission | 1.35% per quarter or part thereof minimum for one quarter. | |
| Guarantee against 100% cash margin | 50% concession on the above rate | |
| Swift Charges | **As Applicable** | |
| Postages | **As Applicable** | |
| Revert of Guarantee before Expiry | **Minimum 1 Qtr BG Commission to be recovered for part of quantum of full guarantee commission to be recovered** | |
| Closure of Guarantee After Expiry of Claim Period | Nil | |
| Invoke of Guarantee | **USD 200 or equivalent in TZS** | |
| | 1. **Financial Guarantees: -**<br>1. In favour of Customs/Excise/Tax Authorities towards tax/Duties payment Etc.<br>2. Favouring Courts for Release of Amounts.<br>3. For Guaranteeing Loan payments.<br>2. **Performance Guarantees: -**<br>1. In lieu of earnest money deposit<br>2. In lieu of tender deposit<br>3. In lieu of security deposit<br>4. To obtain advance payments (generally exports)<br>5. To obtain mobilization advance (generally domestic)<br>6. Towards Direct/indirect taxes to govt. in respect of specific transaction.<br>7. For Direct/indirect taxes disputes with tax Authorities.<br>8. For payment for supplies/services made /rendered<br>9. For Securing retention amount<br>10. For Bidding/tendering for Project Contacts<br>11. For Performance in terms of any agreed contact.<br>**Note: - No processing charges or documentation charges are to be levied in case of Casual BG limits issued against 100% or more cash margin.** | |
| **Imports :-** | | |
| LC Opening charges | 1.35% per quarter +SWIFT charges USD 30/- | 1.35% per quarter +SWIFT charges USD 75/- |
| Against 100% cash margin | 50% concession on the above rate i.e. 0.67% per quarter +SWIFT charges USD 30/- | 50% concession on the above rate i.e. 0.67% per quarter +SWIFT charges USD 75/- |
| LC Amendment Charges | Per amendment 0.40% of LC amount (minimum USD 60 and Maximum USD 325) +SWIFT charges USD 30 (Same for LC against 100% cash margin) | |
| Acceptance of bills under LC | 0.60% of Bill amount Min USD 30 Maximum USD 180 | |
| Retirement of bills under LC | 0.60% of Bill amount Min USD 30 Maximum USD 360 | |
| Inward Bills for Collection | 0.30% of Bill amount minimum USD 150 | |
| **Exports:-** | | |
| Negotiation of Bills under LC | 0.60% of Bill amount Minimum USD30 Maximum USD 360 | |
| Confirmation of Export LC | 0.90% per quarter +SWIFT charges USD 30/- | |
| LC Advising Charges | USD 150 | |
| Export Bills for Collection | 0.60% of Bill amount Minimum USD 30 Max USD 360. | |
| Charges for Certifying invoices subsequent to negotiation | **USD 10 Per Invoice** | |
| Clean payment Received under LC | **USD 100 per occasion** | |
| Advice of transfer in transferable LC | **USD 100 per advice of transfer and acceptance commission at 0.30% Minimum USD 100** | |

### OTHER DISCLOSURES
### (VIAMBATANISHI NYINGINEZO)

| No. | ITEM/TRANSACTION | USD | TSHS |
|---|---|---|---|
| 1.0 | **Base or Prime Lending rate** | 7.50% p.a. | 14.50% p.a. |
| 2.0 | **Maximum Spread above Base or Prime Lending rate** | 7.00% | 7.00% |
| 3.0 | **Penal interest** | | |
| a) | For Non Compliance of Terms of sanction | 3% p.a. over Regular Rate of Interest | |
| b) | For Overdrawing/ Excess Drawings due to non – payment of interest/ Instalments/ Charges | 5% p.a. over Regular Rate of Interest | |
| 4.0 | **Deposit Rate** | | |
| i) | Current Deposit | Nil | Nil |
| ii) | Savings Bank Deposit | 0.50% p.a. | 2.50% p.a. |
| iii) | Fixed/Recurring/QIC/MIC deposit | Up to USD 10,000 | Up to TZS 10,000,000 |
| | 6 months | 2.50% | 6.25% |
| | Over 6 months | 3.00% | 7.25% |
| | | Over USD 10,000 | Over TZS 10,000,000 |
| | 6 months | 3.00% | 6.75% |
| | Over 6 months | 3.50% | 7.75% |
| | * No interest is payable in case of premature withdrawal of fixed deposits | | |

**No Penalties & Other sanctions have been imposed by Bank of Tanzania (BOT)during the Period covered by the Disclosure**

We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information.

| | Name. | Designation | Signature | Date |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Antaryami Sarangi | Managing Director | Signed | 06.07.2023 |
| 2. | Heriabdiel Ayoh | General Manager | Signed | 06.07.2023 |
| 3. | Robert Kibona | General Manager | Signed | 06.07.2023 |

# TFS kuuza asali nchini China

**Na Elizabeth Zaya**

WAKALA wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) unatarajiwa kuingia makubaliano ya kuuza asali China.

Jana, Kamishna wa Uhifadhi wa TFS, Prof. Dos Santos Silayo, alibainisha hayo kwa waandishi wa habari baada ya kutembelea Maonyesho ya 47 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF), maarufu Sabasaba.

Alisema tayari wawekezaji wengi wamevutiwa kuwekeza Tanzania katika sekta hiyo na msukumo wa kufanya hivyo umetokana na ushawishi mkubwa uliofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan kimataifa.

"Kutokana na uongozi thabiti wa Rais Samia Suluhu Hassan, wawekezaji wengi wamevutiwa kuja kuwekeza nchini katika sekta ya misitu na nyuki, ambayo tumepokea uwekezaji mkubwa.

"Wapo wadau wetu wa ndani ambao wanawekeza katika ufugaji lakini wapo ambao wamewekeza kwenye kufanya biashara za nje.

"Tumepata masoko makubwa sana katika Bara la Asia na hivi karibuni tutatia saini makubaliano ya kuingiza asali kwa kiwango kikubwa sana katika soko la China na wanahitaji takribani tani 200,000 kwa mwaka.

"Kwa hiyo, ni soko kubwa sana ambalo tunawahimiza wadau wetu kwamba jambo la kwanza wajitahidi ubora wa mazao tunayozalisha uwe ni wa kiwango cha juu ili tusije kuharibu masoko yetu.

"Lakini tuzalishe kwa kiwango kikubwa kwa sababu sasa hivi uzalishaji uko chini. Tuzalishe asali kutoka katika ikolojia mbalimbali, nyuki aina mbalimbali na mahitaji tofauti," alifafanua.

Kamishna Silayo alisema tayari wameweka nguvu kubwa kwa umma kuhakikisha unajihusisha na ufugaji nyuki na kuzalisha asali yenye viwango kwa makundi yote.

Pia alisema watahakikisha wanaongeza ubora wa mnyororo wenyewe wa biashara kuanzia uchakataji na biashara ya ndani na nje ya nchi.

"Na tumepata masoko makubwa na mengi ni nje ya nchi. Kwa hiyo, wadau wetu wa ndani wanaofanya biashara za kimataifa, ni wajibu wao kuyakaribia masoko hayo ili wapate kipato wao na taifa.

"Lakini na ukubwa wenyewe wa sekta ya nyuki ni jambo ambalo tunalipa msukumo mkubwa, ambapo kwa masoko ambayo tumeyafanyia tathmini pamoja na tathmini yetu ya ubora wa mazao ya nyuki nchini, zinakidhi kabisa uhitaji wa masoko ya nje. Kwa hiyo, fursa iliyopo sasa ni kwa wadau wetu kuongeza jitihada za uzalishaji na biashara kwa ujumla wake," alisema.

Kamishna Silayo pia alisema Tanzania kwa miaka ya hivi karibuni, imeongeza kiwango cha uwekezaji wa ndani na kwa sasa wanasafirisha zaidi mazao ya misitu nje ya nchi kulinganisha na ilivyokuwa awali.

"Miaka mitano iliyopita tulikuwa tunasafirisha mita za ujazo 25,000 za mazao ya misitu kwenda nje na tunaingiza takribani mita za ujazo 110,000 za mazao mbalimbali ya misitu, lakini kwa sasa tunatoa zaidi ya mita za ujazo 95,000 kwenda nje na tunapokea kiasi kidogo takribani mita 30,000 tu.

"Kwa hiyo, tumefanya mageuzi makubwa katika eneo hili kwa sababu ya uwekezaji uliofanywa ndani ya nchi.

"Ukiangalia viwanda vilivyowekezwa ndani vimeleta teknolojia ambazo hazikuzoeleka hapo kabla, ambazo zimezalishaji bidhaa mbalimbali zaidi ya mbao," alisema.

## Wanafunzi UDSM wabuni mashine kukausha mazao ya baharini, ziwani

**Na Christina Mwakangale**

CHUO Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kimebuni mashine ya kisasa kwa ajili ya kukausha mazao ya baharini na ziwani.

Mashine hiyo inaelezwa kuwa na uwezo wa kukausha dagaa kilo 12 kwa nusu siku kulinganishwa na mfumo unaotumiwa sasa na wavuvi wengi hukausha zao hilo, kwa kutumia moshi au kuanika juani kwenye mchanga.

Mbunifu mwenza wa mashine hiyo na mwanafunzi wa chuo hicho, Kelvin Edson, alieleza utendaji kazi wa mashine hiyo alipozungumza na mwandishi katika Banda la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kwenye Maonesho ya Sabasaba jana.

Alisema utafiti walioufanya awali pamoja na mbunifu mwenzie, Samwel Malembo, wote wanafunzi wa Shahada ya Uhandisi Umeme, mwaka wa tatu chuoni huko, walibaini wavuvi hupata vikwazo vya teknolojia na miundombinu ya ukaushiaji dagaa, hususan wakati wa masika.

"Msimu wa mvua, jua hupatikana kwa saa chache na hivyo kusababisha dagaa kuvunda au kuharibika. Baadhi huanika dagaa chini na kuwa na kiwango kikubwa cha mchanga, mawe, si salama kiafya," alisema Kelvin.

Alifafanua matumizi ya mashine hiyo kuwa ni rahisi na inaweza kutumiwa na mtu mwenye kiwango cha uelewa wa kawaida, kwa kuwa hutumia nishati ya umeme wa volti 240 au jua, kisha huwashwa kitufe cha mtambo huo, ambacho huruhusu joto.

"Mtu yeyote anaweza kuendesha mashine hii. Hii bidhaa ni mradi mpya tumeitambulisha katika maonesho haya. Mashine hii inaweza kutumika Ziwa Tanganyika, Victoria na kwingineko, wavuvi wasitegemee tu jua. Tunatarajia kutengeneza mashine kubwa yenye uwezo wa kubeba kilo nyingi za dagaa kwa pamoja," alisema Kelvin.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (kulia), akikabidhi kombe kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Azania, Esther Mang'enya (kushoto), baada ya benki hiyo kuibuka mshindi wa pili wa jumla katika Maonyesho ya 47 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam yanayoendelea hivi sasa jijini humo. Katikati (mwenye miwani) ni Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar, Omar Said Shaaban na Naibu Waziri wa Sanaa, Michezo na Utamaduni, Hamisi Mwinjuma (kulia). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RITA yawaita wananchi Sabasaba ikiwasajili 3,000

**Na Mary Geofrey**

WAKALA wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) umewaomba wananchi kujitokeza kwa wingi katika banda la kwenye Maonesho ya Sabasaba ili kusajiliwa na kupata vyeti vya kuzaliwa papo hapo.


Tangu maonyesho hayo yalipoanza Juni 28, mwaka huu, Watanzania 3,000 wamesajiliwa katika banda la RITA.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa RITA, Frank Kanyusi, alitoa rai hiyo jana alipozungumza na waandishi wa habari waliotembelea banda la wakala huo kupata maelezo ya huduma zinazotolewa.

"Elimu ambayo tumekuwa tukitoa kwa wananchi imekuwa na tija kwani wananchi wameelewa umuhimu wa kuwa na cheti cha kuzaliwa na hivyo wamejitokeza kwa wingi wakiwa na viambatanisho vinavyohitajika na hivyo kufanya usajili kuchukua muda mfupi," alisema Kanyusi.

Alisema viambatanisho muhimu vinavyohitajika ili kufanikisha upatikanaji wa cheti ni kadi ya kliniki, pasi ya kusafiria, cheti cha ubatizo, cheti cha elimu ya msingi au sekondari au vitambulisho vya kupiga kura au utaifa vya wazazi na kitambulisho cha kupiga kura au kitambulisho cha utaifa. Alisema cheti cha kuzaliwa ni nyaraka muhimu kwa kila mwananchi kwa kuwa ni utambulisho wa awali na kiambatanisho kinachomwezesha mwananchi kupata huduma mbalimbali ikiwamo elimu, matibabu, huduma za kifedha, ajira na kuwezesha kupata nyaraka nyingine za utambulisho kama kitambulisho cha Taifa, pasi ya kusafiria na nyinginezo.

Kanyusi alisema miongoni mwa huduma wanazozitoa ni elimu kwa wananchi kuhusu huduma zote ambazo wakala unazitoa zikiwamo huduma ya usajili wa vizazi kwa wananchi ili wapate vyeti vya kuzaliwa sambamba na huduma ya msaada wa kisheria kuhusu masuala ya mirathi na kuandika wosia. Mmoja wa wananchi walionufaika na huduma za RITA, Mary Ishengoma, mbali ya kupongeza huduma, alisema mikakati iliyopo ya kuhakikisha kila Mtanzania anapata na cheti ni hatua nzuri.



# St. Mary Goreti yapongezwa ukuzaji elimu, kuijali jamii

**Na Mwandishi Wetu**

MBUNGE wa Moshi Mjini, Priscus Tarimo, ameupongeza uongozi wa Shule ya Sekondari ya St. Maria Goreti kwa mchangao mkubwa inayotoa katika kukuza sekta ya elimu na katika jamii.

Alitoa pongezi hizo wakati wa kambi maalum ya kupima afya na kuchangia damu iliyoandaliwa na uongozi wa shule hiyo ikiwa ni sehemu ya maadhimisho yanayoendelea ya miaka 25 tangu kuanzishwa kwa shule hiyo.

"Shule hii ilianza kama shule ya sekondari ya kawaida, baadaye ikawa ya hadi kidato cha sita; sasa hivi uongozi wa shule hii umeanzisha shule ya awali pamoja na ya msingi, haya ni mafanikio makubwa kwa shule yenu na mchango mkubwa katika kukuza sekta ya elimu hapa nchini," alisema.

Aidha, aliupongeza uongozi wa shule hiyo kwa kuchangia maboresho ya mazingira mkoani Kilimanjaro kwa kuchangia miche ya miti na uandaaji wa miti katika wilaya zote za mkoa kama sehemu ya maadhimisho.

Kuhusu kambi hiyo, Tarimo alisema pia ni njia nzuri kama sehemu ya maadhimisho ya Jubilei ya miaka 25 ya shule ambapo alisema wananchi watapata fursa ya kuchangia damu ili kuokoa maisha ya wananchi wengine sambamba na kupima hali zao za afya bure.

Tarimo ambaye katika hafla hiyo alijisajili kama mshiriki wa mbio zilizoandaliwa kama sehemu ya maadhimisho hayo, pia aliupongeza uongozi wa shule hiyo kwa kuandaa mbio hizo ambazo alisema zitachangia kuboresha maisha ya washiriki sambamba na kukuza sekta ya michezo.

Mkuu wa Shule ya Sekondari ya St. Maria Goreti, Sr Clementina Kachweka, alisema kambi hiyo imeandaliwa kwa ajili ya kuchangia damu kwa wahitaji, haswa ikitiliwa maanani mahitaji ya damu yamekuwa ni makubwa katika taasisi za tiba mkoani Kilimanjaro.

Aliishukuru Hospitali ya KCMC ya Moshi kwa kuwa mstari wa mbele katika kuratibu zoezi hilo la upimaji afya na kuchangia damu huku wakisaidiwa na wataalamu wengine kutoka Hospitali ya St. Joseph, Hospitali ya Huruma na Manispaa ya Moshi.

Alisema kuwa mbali na zoezi hilo, pia tayari uongozi wa shule hiyo umeshafanya matukio mengine ikiwamo uzinduzi wa maadhimisho hayo ya miaka 25 tangu kuanzishwa kwa shule hiyo na ugawaji wa miti 2,000 kwa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro ambayo itapandwa maeneo mbalimbali mkoani humo.

Shughuli za kuelekea Jubilee ya miaka 25 ya St. Mary Goreti zinaratibiwa na kampuni ya Executive Solutions Ltd, moja ya kampuni zinazoongoza katika kuratibu matukio na masuala ya habari.

# NaCoNGO 'lawashtaki' MaDC, MaDED kwa RC

**Na Godfrey Mushi,**
MOSHI

BARAZA la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO), limewasilisha ombi la kuitaka serikali kuwakemea wakuu wa wilaya na wakurugenzi wa halmashauri kuacha kuwaita wadau wa mashirika hayo kwamba ni 'watu wa makosa'.

Mwenyekiti wa NaCoNGO Taifa, Dk. Lilian Badi, alimweleza hayo Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, mwishoni mwa wiki wakati wa kikao cha mwaka cha Jukwaa la NGOs kilichoratibiwa na baraza hilo.

"Wadau sisi, tunafahamu baadhi yetu walikiuka taratibu za utendaji wao wa kazi, lakini tunafahamu serikali ina macho makubwa iliwamulika ikaona na ikawachukulia hatua.

...Lakini tunapoongea sasa, wana NGOs (mashirika yasiyo ya kiserikali) tunaitwa wakiukwaji wa maadili. Tunaomba sana tusiharibiwe jina letu, kwa sababu ya wenzetu wachache ambao wamekosea ndani ya utekelezaji wao wa kazi. Ninalisema hili kwa sababu ninatambua kwenye wilaya zako, ziko wilaya ambazo zimekumbana na changamoto."

Zaidi, Dk. Badi alisema: "Kama tunakosea, taratibu za kisheria zichukuliwe vizuri, lakini siyo sekta nzima tuwekwe kapu moja kama wakosaji."

Akijibu ombi hilo, Mkuu huyo wa Mkoa, alisema imani yake inamwonyesha kwamba NGOs zinafanya kazi yake kwa kutekeleza sheria, miongozo, kanuni na taratibu za mashirika ambayo wamejiwekea.

"Mkoa wa Kilimanjaro, tutawapa ushirikiano asilimia 100 lakini msijiingize katika kutumika vibaya. Wengine mnatumika vibaya baadhi yenu.

"Wewe sio mwanasiasa, unataka siasa ya nini? Kama unataka siasa acha NGOs, nenda tukapambane kwenye majukwaa kama unataka," alisema.

Babu, aliahidi kukutana na wakuu wote sita wa wilaya na wakurugenzi na kuwapa maelekezo kufanya kazi kwa karibu na NGOs, kwa kuwa yeye ana imani nazo, kwa namna zinavyomsaidia Rais Samia Suluhu Hassan, kutekeleza miradi mbalimbali na kutoa elimu kwa umma.

Awali, Msajili Msaidizi wa NGOs, Mkoa wa Kilimanjaro, Jesca Nyaki, akizungumza katika jukwaa hilo, alisema mashirika hayo yana mchango mkubwa katika mkoa mkoa huo, kwa kuwa mwaka 2022, yametekeleza shughuli mblimbali ambazo zina thamani ya Sh. bilioni 6.1.





**KOZI YA WAFANYAKAZI NDANI YA NDEGE (CABIN CREW).**

Chuo Cha Kampuni ya Ndege ya Tanzania (ATCL Training Center ) kina furaha kuwatangazia watanzania wote kuwa kwa mara nyingine kitaendesha kozi ya wahudumu ndani ya ndege (Cabin Crew ) kuanzia tarehe 04 September 2023. Kozi hii ni ya muda wa miezi mitatu (03), chuo kipo uwanja wa ndege wa kimataifa wa Julius Nyerere-Dar es salaam (JNIA) Terminal One kwenye jengo la utawala la ATCL karibu kabisa na kituo cha polisi uwanja wa ndege. Chuo kinakaribisha maombi ya kujiunga na kozi hii kwa wenye sifa zilizoainishwa hapo chini. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 09 August 2023.

**Sifa za mwombaji.**

i. Awe na umri kuanzia miaka 18 hadi miaka 25
ii. Awe timamu kiakili, kimaumbile na urefu kuanzia sentimita 161/ futi 5"4 na kuendelea
iii. Elimu sio chini ya kidato cha nne na kufaulu angalao masomo manne, hasa masomo ya Kiingereza na Jiografia
iv. Aweze kuongea na kuandika kwa ufasaha lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Muombaji mwenye uelewa wa lugha zaidi ya hizi mbili kama Kiarabu, Kichina, Kihindi na Kifaransa atapewa kipaumbele.
v. Awe Mtanzania au raia wa kigeni mwenye vibali halali vinavyomruhusu kukaa na kusoma nchini.


**Angalizo:** Waombaji kutoka nchi za kigeni watatakiwa kulinganisha matokeo ya vyeti vyao kwenye Baraza la Mitihani Tanzania (NACTE) yafanane na matokeo ya Tanzania.

**Barua ya maombi iambatane na vitu vifuatavyo.**

i. Nakala za vyeti vya shule/chuo alikosoma
ii. Nakala ya cheti cha kuzaliwa
iii. Picha mbili ndogo (passport size) na picha moja yenye kuonyesha umbo lote ukubwa wa 6x8 "inchi"
iv. Curriculum Vitae –CV

**Maombi yatumwe kwa:**
**Principal**
**ATCL Training Center**
**Box no 543**
**Dar**
**Email, training@airtanzania.co.tz**
**Mob: +255735787212 , Landline: +255222842543**
**ATCL TRAINING CENTER**

*Welcomes you, to where you can Fly*





# Wafugaji nyuki waomba kurejeshewa mizinga waliyopokwa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAFUGAJI wa nyuki kutoka Kata ya Ulowa Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga, wameiomba serikali kuwarejeshea mizanga yao zaidi ya 60,000 iliyochukuliwa baada ya kufutwa kwa Hifadhi ya Kigosi Moyowosi waliyokuwa wakilitumia kufuga nyuki.

Hifadhi hiyo ya Kigosi iliyowekwa chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Hifadhi ya Taifa (TANAPA) kisha kutoa siku 10 kwa wafugaji hao zaidi 15,000 kuchukua mizinga yao hali iliyokuwa ngumu kutokana na mizinga hiyo kuwa mingi na kushindwa kuiondoa kwa wakati.

Mwenyeki wa umoja wa wafugaji hao wa nyuki, John Jeremiah, aliyabainisha hayo jana katika mkutano wa hadhara wa Mbunge wa Ushetu, Emmanuel Cherehani na kuhudhuriwa na Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi, Livingstone Lusinde kutoka Mtera.

Alisema kuwa kupitia mizinga hiyo walitarajia kuzalisha zaidi ya lita za asali 15,000 hadi 20,000 lakini zilibakishwa kwenye hifadhi hiyo na kurudisha nyuma maendeleo ya wafugaji hao waliounda kikundi ili kujikwamua kiuchumi.

Alisema baada ya kushindwa kuondoa mizinga hiyo walianzisha ufugaji upya katika Pori la Ubagwe-Ushetu kwa kuanza na mizinga 20,000 na asali iliyopatikana ilikuwa sio bora kama iliyokuwa inapatikana katika Hifadhi ya Kigosi Moyowosi kwani mizinga inahitaji kuweka umbali wa kilometa 15 na kulikuwa na mji ya kutosha kwasababu ya uwepo wa mito ndani yake.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Ushetu ambaye ni Diwani wa Nyankende, Doa Limbu alisema, mgogoro wa pori hiyo unazaidi ya miaka 10 licha ya wafugaji wa nyuki kulitumia na wanaomba kurejeshwa chini ya halmashauri ili liwe moja ya chanzo cha mapato ya ndani na siyo kukabidhiwa na kusimamiwa na Wakala wa Misitu Tanzania (TFS).

Alisema, halmashauri ina ng'ombe 216,114, mbuzi 80,000 na kondoo 20,000 na eneo hilo lina ukubwa wa kilometa za mraba 7,000, hivyo linatosha kutumiwa na wafugaji bila kuharibu uoto asili na shughuli nyingine za uvuvi utafanyika kwa sababu ndani yake kuna mito mikubwa yenye samaki wa kila aina.

Kadhalika aliomba Msitu wa Usumba wenye hekta 36,000 unaotambuliwa na GIN 412 ya mwaka 1956 uondolewe kwenye umiliki wa TFS kuwa mali ya halmashauri, ili kuvipatia vikundi 60 vya ufugaji nyuki vya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu ambavyo pia wanaviwezesha mikopo isiyokuwa na riba.

Mbunge wa Ushetu, Emmanuel Cherehani alisema kurejeshwa kwa pori hilo ameshirikiana na wabunge wenzake kwa kumuunga mkono katika hoja aliyokuwa ameiwasilisha bungeni.

Alisema atahakikisha anaifuatilia mizinga hiyo ili kuhakikisha inarejeshwa kwa wafugaji na kuwanufaisha kama ilivyokuwa hapo awali.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi kutoka Mnvumi, Livingstone Lusinde alisema, Ushetu imepokea Sh.bilioni 18 kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo hususani kwenye sekta ya elimu, maji na afya.

Hivyo, aliwataka wasimamizi wa miradi kuhakikisha miradi yote inakamilika kwa wakati na kuwanufaisha wananchi.



Mbunge wa Jimbo la Ushetu mkoani Shinyanga, Emmanuel Cherehani, akiwaeleza wananchi wa jimbo hilo namna alivyoshirikiana na wabunge wenzie katika kujenga hoja na kurejesha Hifadhi ya Taifa ya Kigosi nakuwa poli la akiba Kigosi, wakati wa mkutano wa hadhara uliofanyika Kata ya Ulowa Halmashauri ya Ushetu jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

## UWT Shinyanga watahadharishwa kuhusu makundi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

KATIBU wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Shinyanga Mjini, Ally Majeshi, ameutaka Umoja wa Wanawake wa CCM (UWT), kutokukubali kugawanywa na makundi ya wabunge, bali waendelee kuwa wamoja na kuijenga jumuiya yao na chama.

Alitoa kauli hiyo juzi wakati wa mkutano mkuu wa jumuiya hiyo uliofanyika wilayani humo.

Alisema kuwa bila kujali makundi ya wabunge umoja huo unatakiwa kufanya vikao vya mara kwa mara kuanzia ngazi za matawi lengo likiwa ni kuinua umoja wao.

"Na nyie wabunge mnapofika katika maeneo yenu fanyeni mikutano na kuzipokea kero za wananchi zilizopo na kuzitatua kwa wakati na siyo kufanya kazi ya kuwagawa wajumbe," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wanawake wa CCM (UWT) Wilaya ya Shinyanga Mjini, Rehema Nhamanilo, aliwataka wajumbe wa baraza hilo kuwa na ushirikiano na wabunge wote, kufanya kazi za jumuiya na chama, kusajili wanachama wapya ili uchaguzi ujao chama kipate ushindi wa kishindo.

Aidha, Mbunge wa Viti Maalumu, Christina Mzava, aliwataka wanawake wa UWT kuwa na ushirikiano na wabunge wote lengo likiwa ni kuweka mazingira rafiki katika kutekeleza shughuli za kimaendeleo na kujenga chama.

Alisema: "Huu ni wakati sasa wa kufanya kazi, hivyo tunatakiwa tuache tofauti zetu tufanye kazi mpaka tumalize muda wetu kwa kuacha alama nzuri ya utekelezaji majukumu katika ushirikiano."

# TFRA yataka udhibiti utoroshwaji mbolea kwenda nje

**Na Timothy Itembe,** MARA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Mbolea nchini (TFRA) Kanda ya Ziwa imezitaka mamlaka za kudhibiti usafirishaji wa bidhaa katika maeneo ya mipakani kuhakikisha wanadhibiti utoroshaji wa mbolea ya ruzuku kwenda katika nchi jirani kinyume cha sheria.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Meneja wa TFRA Kanda ya Ziwa, Dk. Asheri Kalala, baada ya semina ya kuwajengea uwezo viongozi wa Chama Kikuu cha Wakulima wa Mkoa Mara (WAMACU) kuhusu sheria na kanuni zambolea ya mwaka 2009.

Meneja huyo alisema peke yao hawataweza kudhibiti utoroshaji wa mbolea ya ruzuku kwenda nchi jirani ikiwamo Kenya mpaka mamlaka zinazosimamia sheria zitakaposhirikiana kukemea pamoja na kuchukua hatua kwa wale wanaopatikana wakitorosha mbolea kimagendo.

Dk. Kalala alisema serikali inampango wa kumkomboa na kumwinua mkulima kupitia mbolea ya ruzuku kwa sababu mbolea inapatikana kwa wingi na kwa bei elekezi ya Sh.70,000 kwa mkulima anayepeleka shambani licha ya kuwapo kwa baadhi ya watu wasio waaminifu wanaotorosha mbolea hiyo na kufanyia shughuli binafsi.

"Tumekuwa tukitoa elimu kwa vyama vikuu vya ushirika nchi nzima kufuatia agizo la Waziri wa Kilimo kututaka kwenda kutoa elimu ya sheria na kanuni za mbolea ya mwaka 2009 kwenye vyama vikuu vya ushirika, kwamba kwa Kanda ya Ziwa tunatoa elimu hiyo katika mikoa sita," alisema Dk. Kalala.

Meneja Mkuu WAMACU, Samwel Gisiboye alisema chama hicho kitahakikisha wakulima wote wanakuwa mabalozi, wanafuata sheria ikiwa ni pamoja na kudhibiti utoroshwaji wake kwenda nje ya nchi.

Aidha, aliwataka wakulima kuchangamkia fursa hiyo ya uwepo wa mbolea ya ruzuku kwa ajili ya matumizi kwa kilimo bora, huku wakiahidi kuisambaza kwenye vituo ili kuwafikia wakulima.

Nipashe
Spotika



WACHEZAJI 10 WA THAMANI ZAIDI DUNIANI KWA SASA 12 - 13




WILLIAM SALIBA

# MABEKI WATATU ARSENAL WANAOWEZA KUWEKWA BENCHI NA JURRIEN TIMBER

**LONDON, England**

KWA mujibu wa Fabrizio Romano, mazungumzo kati ya Arsenal na Ajax kuhusu uwezekano wa kumsajili Jurrien Timber yanakaribia kukamilika. Ameeleza kuwa ada ya uhamisho inaweza kupanda hadi euro milioni 47.

Timber mwenye umri wa miaka 22, ni beki chipukizi anayetumainiwa na uwezo wake wa kufanya mashambulizi muhimu ni bora.

Ustadi wake wa kuendeleza mpira katika mashambulizi pia ni sifa nyingine muhimu ambayo anayo. Katika msimu wa 2022-23, alishinda asilimia 76.2 ya safu yake ya ulinzi na pia alisajili mchango wa mabao manne katika michezo 47.

'Washikabunduki' wanamsajili Mholanzi huyo kwa sababu ya uwezo wake wa kucheza kama beki wa kati na beki wa kulia inapobidi, jambo ambalo ni la ushindi kwa klabu. Mtindo wake wa uchezaji unalingana kabisa na muundo wa kocha Mikel Arteta.

Hata hivyo, kupatikana kwake kunaweza kumaanisha kuwa baadhi ya mabeki wa kati waliopo klabuni hapo wanaweza kuondoka au kuachwa benchi. Acha tuangalie wachezaji watatu ambao wanaweza kuathiriwa ikiwa mpango huo utakamilika...

**#1. Ben White**

Beki hodari ambaye anaweza kuathiriwa na uhamisho huo ni Ben White, kwani ndiye chaguo la kwanza la beki wa kulia wa Washikabunduki hao msimu uliopita.

Wakati wa msimu wa 2022-23, White alifunga mabao mawili na alitoa pasi tano za mabao katika mechi 46 kwenye mashindano yote.

Hata hivyo, kutokana na Timber kuingia kwenye mpambano huo, nafasi yake ya kucheza kama beki wa kulia inaweza kupungua.

Hii inakuja kutokana na ustadi wa Timber kucheza kwenye beki ya kulia pia. Inaweza pia kusemwa kuwa Timber ana ufundi zaidi na wa kutisha katika beki ya kulia kuliko White. Kwa hiyo, wakati wake wa kucheza unaweza kupungua msimu ujao.

**#2. Jakub Kiwior**

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Poland ni beki bora wa kati, na uwezo wake wa kumkaba mpinzani wake katika safu ya ulinzi ni wa ajabu. Zaidi ya hayo, nafasi yake katika ulinzi ni ya hali ya juu pia.

Januari 2023, Washikabunduki walimsajili kutoka Spezia kwa pauni milioni 20, na alicheza mechi nane, na kusaidia kusawazisha mabao mawili kama mchezaji wa Arsenal msimu uliopita.

Ingawa inaweza kutabiriwa kuwa Kiwior ni beki wa kati anayetarajiwa, kuwasili kwa Timber kunaweza kumuacha benchi.

**#3. William Saliba**

William Saliba ni mmoja wa wachezaji bora zaidi wa msimu wa 2022-23, na ustadi wake wa ulinzi uliboresha utendaji wa jumla wa Arsenal pale nyuma.

Mfaransa huyo alicheza mechi 33 kwenye mashindano yote akiwa na Arsenal msimu uliopita. Hata hivyo, beki huyo anayetumia mguu wa kulia alijitahidi kubaki fiti, kwani alikuwa nje ya uwanja kwa mechi 12 mwishoni mwa msimu uliopita.

Kwa kuzingatia kiwango cha Saliba msimu uliopita na umuhimu wake kwa timu, kuna uwezekano mdogo wa Timber kumtoa kwenye kikosi cha kwanza. Hata hivyo, itakuwa ya kuvutia kuona uamuzi wa kocha utakuwa nini ikiwa Saliba atajitahidi kubaki fiti.

## ISIKUPITE

KWA mujibu wa mtandao wa ESPN, Bukayo Saka wa Arsenal ndiye winga bora zaidi akifuatiwa na Khvicha Kvaratskhelia (Napoli), Jack Grealish (Man City), Ousmane Dembélé (Barca), Gabriel Martinelli (Arsenal), Riyad Mahrez (Man City), Kingsley Coman (Bayern), Rodrygo (Madrid), Phil Foden (Man City) na Moussa Diaby (Leverkusen).



Extra Time

# WACHEZAJI 10 WA THAMANI ZAIDI DUNIANI KWA SASA



Haaland

**LONDON, England**

THAMANI ya soko la uhamisho wa mchezaji ni kiashirio kikuu kinachotumiwa na klabu, mawakala na wachambuzi kutathmini thamani na gharama inayowezekana ya mchezaji wakati wa mazungumzo ya uhamisho.

Inachangiwa na mambo mbalimbali, ikiwa ni pamoja na umri wa mchezaji, kiwango cha uchezaji, hali ya mkataba, mahitaji ya soko na mitindo ya jumla ya soko.

Thamani ya soko la mchezaji mara nyingi huamuliwa kwa kuchanganua uhamisho unaolinganishwa, takwimu za mchezaji, sifa ya kimataifa na uwezekano wa ukuaji kwa siku zijazo.

Zaidi ya hayo, mambo kama vile majeraha, uthabiti na kiwango cha ushindani ambamo wanafanya wanaweza pia kuathiri thamani yao.

Makala haya inawangalia wachezaji 10 wenye thamani zaidi duniani kwa sasa, haya sasa...

**#10. Rodrygo Goes (Real Madrid) - Euro Milioni 100**

Rodrygo Goes ni mmoja wa washambuliaji chipukizi wanaosisimua zaidi katika ulimwengu wa soka. Winga huyo wa Real Madrid ni mmoja wa washambuliaji mahiri duniani na anaweza kucheza katika nafasi nyingi kwenye mstari wa mbele.

Winga huyo wa Brazil alikuwa mmoja wa wachezaji bora wa Real Madrid msimu wa 2022-23. Katika mechi 57 kwenye michuano yote akiwa na Real Madrid msimu huu, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, alifunga mabao 19 na kutoa asisti 11. Thamani ya soko la uhamisho la Rodrygo ni euro milioni 100.

**#9. Pedri (Barcelona) - Euro Milioni 100**

Kinda wa Barcelona, Pedri ana umri wa miaka 20 pekee, lakini tayari anachukuliwa kuwa mmoja wa viungo bora zaidi wa kati duniani. Pedri anapendekezwa kuwa kwenye njia za Xavi na Andres Iniesta na ana uwezo na ustadi wa kufanya hivyo.

Tayari amekuwa mchezaji mwenye ushawishi kwa klabu na nchi na ana uhakika wa kuwa na mustakabali mzuri. Pedri ana thamani ya euro milioni 100.

**#8. Phil Foden (Manchester City) - Euro Milioni 110**

Phil Foden ana mchanganyiko wa ajabu wa ustadi wa kiufundi, maono na ubunifu ambao humuweka juu kwenye uwanja wa mpira. Udhibiti wake wa karibu wa mpira, pasi sahihi na uwezo wa kupata nafasi humfanya awe mchezaji wa kutisha.

Akiwa na umri mdogo, Foden tayari ameonesha uwezo mkubwa, na kuendelea kwake kukua kunaonesha kuwa ana uwezo wa kuwa mmoja wa viungo bora duniani katika miaka ijayo, na uwezekano wa kuacha alama isiyofutika kwenye mchezo huo.

**#7. Jamal Musiala (Bayern Munich) - Euro Milioni 110**

Jamal Musiala alitia saini msimu wa 2022-23 kwa kuifungia Bayern Munich bao la ushindi wa taji la Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, katika mchezo wao wa mwisho dhidi ya FC Koln.

Mtindo wa uchezaji wa Musiala unatambulika kwa uwezo wake wa kipekee wa kucheza chenga na udhibiti wa karibu wa mpira, unaomruhusu kupitia nafasi zilizobana na kuwakwepa mabeki kwa urahisi.

Ana ustadi wa asili na ubunifu unaomwezesha kufanya mikimbio mikali, kutoa pasi za mabao muhimu na kuchangia kwa mabao muhimu, na kumfanya kuwa mchezaji wa kuvutia kumtazama uwanjani.

**#6. Victor Osimhen (Napoli) - Euro Milioni 120**

Mshambuliaji wa Nigeria, Victor Osimhen, ameingiza jina lake katika historia ya mji wa Naples kwa kuiwezesha Napoli kutwaa taji lao la kwanza la Ligi Kuu ya Italia, Serie A, kwa kipindi cha miaka 33 msimu huu. Osimhen aliboresha mchezo wake kwa kiasi kikubwa msimu huu na sasa amejidhihirisha kuwa mmoja wa washambuliaji bora zaidi duniani hivi sasa.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, ni mmoja wa wachezaji wanaosakwa zaidi duniani kwa sasa na thamani yake ya soko la uhamisho inafikia euro milioni 120.

**#5. Bukayo Saka (Arsenal) - Euro Milioni 120**

Bukayo Saka ni mmoja wa mawinga bora zaidi duniani. Katika msimu mzima wa 2022-23, alionesha ukomavu wake kwa kuongoza mashambulizi ya Arsenal. Ustadi wa ajabu wa Saka wa kucheza chenga, wepesi na uwezo wa kuvutia wa kupiga mashuti humfanya kuwa hatari kwa beki yeyote katika nafasi ya tatu ya mwisho.

Mwingereza huyo pia amekuwa mchezaji muhimu kwa England kwenye hatua ya kimataifa. Ana thamani ya euro milioni 120.

**#4. Jude Bellingham (Real Madrid) - Euro Milioni 120**

Jude Bellingham, ambaye alikuwa mwanga wa uongozi wa Borussia Dortmund msimu wa 2022-23, amejiunga na Real Madrid msimu huu wa majira ya joto. Mwingereza huyo ana umri wa miaka 19, lakini ukomavu wake na ustadi wake wa kiufundi unakanusha umri wake.

Licha ya umri wake mdogo, anaonesha kiwango cha utulivu na zaidi ya hayo, uwezo wa Bellingham ni wa kuvutia na thamani yake kwa sasa ni euro milioni 120.

**#3. Vinicius Junior (Real Madrid) - Euro Milioni 150**

Vinicius Junior ana mchanganyiko wa kuvutia wa kasi, wepesi na ustadi wa kiufundi ambao unamfanya kuwa tishio la mara kwa mara katika safu ya tatu ya kushambulia. Uwezo wake wa kuchukua mabeki, kutengeneza nafasi na kufunga mabao unaonesha uwezo wake mkubwa kama fowadi mahiri na mwenye mustakabali mzuri mbeleni.

Kutokana na kuondoka kwa Karim Benzema mapema msimu huu wa majira ya joto, Vinicius sasa ndiye mshambulizi mkuu wa Real Madrid. Mchezaji huyo mwenye kipaji cha ajabu ana miaka 22, thamani yake ya soko la uhamisho ni euro milioni 150.

**#2. Kylian Mbappe (Paris Saint-Germain) - Euro Milioni 180**

Kylian Mbappe alifunga hat-trick nzuri katika fainali ya Kombe la Dunia la FIFA la 2022 kwa Ufaransa dhidi ya Argentina na bado akaishia kwenye timu iliyopoteza. Aliondoka na Kiatu cha Dhahabu kwenye mashindano hayo na anachukuliwa kuwa mmoja wa washambuliaji wakubwa wa zama hizi na bado ana umri wa miaka 24 tu.

Mbappe anapendekezwa kushinda tuzo nyingi za Ballon d'Or siku zijazo na kwa sasa thamani yake ni euro milioni 180.

**#1. Erling Haaland (Manchester City) - Euro Milioni 180**

Mashine ya kufunga mabao ya Manchester City, Erling Haaland, huenda ikamshinda Lionel Messi kwenye tuzo ya Ballon d'Or ya 2023 mwaka huu. Kiwango chake cha ajabu kilikuwa muhimu kwa ushindi wa City wa kutwaa mataji matatu msimu huu. Haaland ni mshambuliaji mkali sana na aliye na mpangilio mzuri ambaye kumzuria ni ngumu.

Haaland ana umri wa miaka 22 tu na tayari ndiye mshambuliaji bora zaidi duniani. Thamani yake ya soko la uhamisho inasimama kwenye euro milioni 180.

## Nukuu


"Jinsi anavyoshughulika na mambo kwa upole na msaada anaoutoa kwa watu wake katika nchi yake ni ya kushangaza sana. Siku nyingine huwa nakereka nikisoma vyombo vya habari kuhusu yeye na mwandishi wa habari akimuuliza kwa nini huna Ferrari', na anasema, 'Hapana, sihitaji. Napendelea kuwa na gari la kawaida'. Miezi miwili baadaye tunamwona. Amekuwa akifanya mambo nchini mwake. Ni mfano mkubwa," **Nyota wa zamani wa Ivory Coast na Man City, Yaya Toure, akimsifu raia mwenza na mchezaji wa Bayern Munich, Sadio Mane kwa kazi yake nzuri nje ya soka.**



"Messi au Ronaldo? Sijui kwa nini unaniuliza hivi kila wakati. Utapata jibu lile lile: Leo Messi," **Mshambuliaji wa Manchester City, Erling Haaland, alipoulizwa nani bora kwake kati ya Lionel Messi na Cristiano Ronaldo.**




"[Luka] Modric alimpigia simu Arda na kusema: 'Nitastaafu baada ya mwaka mmoja; jezi namba 10 itakuwa yako," **Baba mzazi wa kinda mpya wa Real Madrid, Arda Guler aliyejiunga na timu hiyo akitokea Fenerbahce.**





# NYOTA WAPYA LIGI KUU BARA WANAOTARAJIWA KUTIKISA 2023/24

Che Malone

**Na Adam Fungamwango**

MAMBO yamezidi kupamba moto ambapo viongozi wa klabu mbalimbali nchini wanapishana, wengine kupigana vikumbo kwenye Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere kupokea wageni ambao ni wachezaji wanaokuja kusaini mikataba, kabla ya kuanza kuzitumikia timu hizo.

Ndani nako kumekuwa na purukushani ya wachezaji kutoka upande huu kwenda mwingine, ili mradi tu kila klabu inataka wachezaji ambao zinaamini wanaweza kuwapa kitu tofauti kwa msimu ujao wa mashindano, hasa Ligi Kuu ambayo inatarajiwa kuwa kali na ya kusisimua.

Baada ya tetesi nyingi za usajili nchini hatimaye klabu zimeanza kutangaza rasmi wachezaji wao watakaowatumia msimu ujao.

Ingawa bado zinaendelea na usajili, lakini mashabiki wa soka wameanza kushusha presha zao baada ya kipindi kirefu cha tetesi.

Klabu zimekuwa zikiangusha moja moja kwa kuwatangaza wachezaji wapya ambao ndiyo kiu kubwa kwa mashabiki wao.

Kwenye makala haya, tumekukusanyia majina ya wachezaji wale tu ambao tayari wametangazwa rasmi kusajiliwa na klabu zao, na si tetesi tena...

**Feisal Salum - Azam FC**

Anaweka rekodi ya kuwa mchezaji wa kwanza kwenye klabu zote nchini kusajiliwa na kutangazwa rasmi, baada ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, kuingilia kati suala lake.

Feisal Salum alitangazwa kusajiliwa na Azam FC mwanzoni mwa mwezi uliopita, baada ya sintofahamu ya muda mrefu kati yake na Klabu ya Yanga aliyokuwa akiichezea awali.

Mzozo huo ulianza tangu Desemba mwaka jana alipokuwa akishinikiza kuondoka klabu hapo, lakini Yanga iliweka ngumu na hata kesi yao ilipokuwa ikipelekwa kwenye Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji, mchezaji huyo alitakiwa kurejea kwenye klabu yake ambayo yeye mwenyewe hakuridhia tena kurejea.

Wakati akijiandaa kwenye Mahakama ya Juu ya Usuluhishi ya Migogoro ya Michezo (CAS), ndipo rais alipoingilia kati akiwataka Yanga kukaa na mchezaji wao kumalizana, alipowaalika Ikulu kwa chakula cha jioni kuwapongeza kwa kufika fainali ya Kombe la Shirikisho Barani Afrika. Ataonekana msimu ujao akiwa amevalia jezi namba sita kwenye klabu yake mpya ya Azam FC.

**Nickson Kibabage - Yanga**

Ni mchezaji wa kwanza kutangazwa rasmi na Klabu ya Yanga msimu huu akitokea Singida Fountain Gate

Kibabage anakwenda kuchukua namba ya David Brayson ambaye huenda akaonyeshwa mlango wa kutokea, hivyo kwenda kugombea namba na beki wa Kikongomani, Joyce Lomalisa.

Ameichezea Singida Big Stars kwa kipindi cha nusu msimu akisajiliwa kutoka Mtibwa kwenye dirisha la dogo la usajili Desemba mwaka jana.

Hata hivyo, alikuwa amerejea kutoka Difaa El Jadidi ya Morocco alikokwenda kucheza soka la kulipwa 2019, baadaye akapelekwa kwa mkopo Klabu ya Youssoufia Berrechi ya nchini humo kabla ya kurejea Mtibwa.

**Willy Essomba Onana - Simba**

Klabu ya Simba nayo imemtangaza mchezaji wake wa kwanza msimu huu, Wlly Essomba Onana, akitokea Rayon Sport ya Rwanda ambako alimaliza ligi akiwa mfungaji bora na mabao ya 16, 'assist' tano, akiwa pia mchezaji bora wa msimu uliomalizika, MVP.

Raia huyo wa Cameroon, amesaini mkataba wa miaka miwili, na mbali na nafasi yake ya asili kuwa ni winga wa kushoto, ana uwezo wa kucheza pia winga ya kulia pamoja na mshambuliaji msaidizi, namba 10.

**Djibril Sillah - Azam FC**

Azam imemsajili kiungo mshambuliaji Djibril Sillah kutoka Raja Athletic Club ya Casablanca nchini Morocco.

Msimu uliopita kwenye Ligi Kuu Morocco, Sillah, raia wa Gambia alifanikiwa kufunga jumla ya mabao saba na kutoa pasi za mwisho nne, wakati akiwa kwa mkopo JS Soualem.

**Aubin Kramo Kouame - Simba**

Mchezaji mwingine aliyeshtua usajili wa Tanzania ni Aubin Kramo Kouame akitokea Asec Mimosas ya Ivory Coast. Ana uwezo wa kucheza winga zote mbili, na alifunga mabao matatu kwenye mechi tatu za Ligi ya Mabingwa Afrika na manne Kombe la Shirikisho Afrika katika mechi 10 ambazo timu yake imecheza msimu uliopita.

Historia yake inaonyesha kuwa alianza kucheza soka la ushindani kwenye klabu hiyo ya Asec Mimosas mwaka 2015, kabla ya kutimkia Africa Sports ya nchi humo 2017, lakini 2019, akaondoka kwenye klabu hiyo akihamia FC San Pedro ya nchini humo humo mpaka 2021 aliporejea Asec Mimosas, kabla ya Simba kumsajili kwa ajili ya msimu ujao.

**Alassane Diao - Azam FC**

Azam haikupoa, badala yake ilishusha chumba kingine raia wa Senegal, bonge la straika 'mbavu nene.'

Amesajiliwa kwa mkataba wa miaka miwili ili kuwapa changamoto Mzimbabwe Idris Mbombo na Mzimbabwe, Prince Dube mwenye eneo la ushambuliaji. Diao anatokea Klabu ya US Goree ya Dakar, Senegal.

**Joash Onyango - Singida Fountain Gate**

Ukiondoa Klabu za Simba, Yanga na Azam FC, klabu ya kwanza nje ya hizo ambazo usajili wake umekamilika na kutangazwa rasmi ni wa Joash Ongango.

Amekamilisha usajili wa mkopo kutoka Simba kwenda Singida Fountaine Gate ili kupeleka uzoefu wake wa mechi za kimataifa akiwa na klabu hiyo kwenda timu yake mpya ambayo kwa mara ya kwanza itashiriki Kombe la Shirikisho Afrika.

**Che Malone Fondoh - Simba**

Jana mchana, Klabu ya Simba ilimtangaza mchezaji wake mpya wa tatu msimu huu, Che Malone Fondoh, raia wa Cameroon anayecheza nafasi ya beki wa kati.

Hivi majuzi ametajwa kuwa ni beki bora kwenye Ligi Kuu ya nchi hiyo, akiichezea Cotonsport na ilibidi Simba kukaza msuli kumpata kwani alikuwa akiwaniwa na klabu mbalimbali za Afrika na Ulaya, ikiwamo FC Zurich ya Uswisi.

Licha ya kwamba inaonekana anasajiliwa baada ya kuondoka kwa Mohamed Ouattara, lakini ni mchezaji anayeonekana kwenda kuingia moja kwa moja kwenye kikosi cha timu hiyo baada ya kuondoka kwa Joash Onyango aliyeelekea Singida Fountaine Gate kwa mkopo.

**JE, WAJUA?**



KWA mujibu wa mtandao wa ESPN, makipa 10 bora kwa sasa ni Thibaut Courtois (Madrid), Marc-André ter Stegen (Barca), Alisson Becker (Liverpool), Mike Maignan (Milan), Jan Oblak (Atletico),Gianluigi Donnarumma (PSG), Ederson (City), Aaron Ramsdale (Arsenal), Emiliano Martínez (Aston Villa) na Nick Pope (Newcastle).



# Ofisa Ustawi wa Jamii ataja kiini wenye ulemavu kunyimwa haki

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

UELEWA mdogo kwa baadhi ya wazazi na walezi nchini kuhusu haki za watoto wenye ulemavu kumetajwa kuwa chanzo cha wengi kutopata haki zao za msingi ikiwamo elimu.

Ofisa Ustawi wa Jamii Jiji la Dodoma, Mboni Msantu, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na wazazi na walezi wenye watoto hao kwenye mafunzo ya uhamasishaji jamii juu ya masuala ya elimu jumuishi na ukusanyaji wa taarifa za matukio ya unyanyasaji na ukatili dhidi ya wenye ulemavu yaliyofanyika Kata ya Nkulabi jijini humo.

Alisema kwenye kata hiyo wamegundua watoto 16 wenye ulemavu wanaostahili kuandikishwa na kupelekwa shule hawajaenda na bado wamefichwa majumbani na kuwasababishia kukosa haki hiyo ya msingi ya elimu.

Msantu alisema miongoni mwa familia zenye watoto ambao wana ulemavu bado uelewa wao ni mdogo wa kuona umuhimu wa kuwasomesha.

Mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama vya Watu wenye Ulemavu (SHIVYAWATA) Mkoa wa Dodoma, Omar Lubuva, aliwataka wadau kuzisaidia familia zisizojiweza misaada mbalimbali ikiwamo ya kielimu kiafya, chakula na mavazi.

Alisema baadhi ya wazazi na walezi wameshindwa kuwapeleka shule kutokana na kero zinazowakabili.

Naye Mratibu wa Mradi wa Elimu Jumuishi unaosimamiwa na Kanisa la Free Pentecostel Church of Tanzania (FPCT), Janne Mgidange, aliwataka wazazi wenye watoto hao ambao wana ulemavu kuepukana na mapokeo ya imani potofu na kuwasababishia kuwanyima haki kupata elimu.

Alisema bado kuna baadhi ya wazazi na walezi wanaoamini kuwa watoto wenye ulemavu ni kama wana mikosi na hawastahili kusomeshwa imani kama hiyo ni ukatili na inawaongezea umaskini zaidi kwa kukosa elimu.

Mmoja wazazi, Rozi Ristal aliomba elimu zaidi itolewe na kutoa adhabu kwa wale wanaoendelea kuwaficha badala ya kuwaandikisha na kuwapeleka shule.

Alisema: "Tuwaombe wadau mbalimbali wa maendeleo ya elimu, kupitia miradi yao ikiwamo elimu jumuishi, Shivyawata, viongozi wa serikali mashirika na taasisi za kidini kuendelea uhamasishaji kwa wazazi, ili wasikubali kujiongezea umaskini kwa kuwaweka na kuwaficha watoto hao majumbani".



Mwenyekiti wa SHIVYAWATA Mkoa wa Dodoma, Omar Lubuva (kulia), akimkabidhi Sara George, kifaa kisaidizi cha kutembelea baada ya kumalizika kwa mafunzo ya kuhamasisha jamii juu ya elimu jumuishi na kukusanya taarifa za watoto wenye ulemavu katika Kata ya Nkulabi, Mtaa wa Mwongozi jijini Dodoma jana. Wa pili kulia ni Katibu wa SHIVYAWATA Dodoma, Justus Ng'wantalima. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# DC aagiza watendaji kutumia sensa kupanga maendeleo

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKUU wa Wilaya ya Singida, Mhandisi Paskas Muragili, amewaagiza viongozi na watendaji wilayani humo kutumia matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 kufanya maamuzi na kutathmini utekelezaji wa mipango ya maendeleo.

Muragili alitoa agizo hilo jana alipokuwa akifungua mafunzo ya usambazaji na matumizi ya matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 kwa viongozi yaliyofanyika mjini Singida.

Alisema serikali imeamua kutoa mafunzo hayo kwa wadau mbalimbali katika ngazi mbalimbali za kiutawala kuhusu namna ya kutumia matokeo ya sensa ili kuwapa uwezo wa kushiriki katika kufanya maamuzi yanayohusu sera na mipango ya maendeleo ya wananchi kwa kuwa wapo karibu nao.

Meneja wa Takwimu Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) Mkoa wa Singida, Naing'oya Kipuyo, akizungumza kwa niaba ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Dk. Albina Chuwa alisema mafunzo hayo ni mfufulizo wa mafunzo ya matumizi ya matokeo ya sensa kwa makundi mbalimbali katika jamii yanayoendeshwa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar.

Kipuyo alisema madhumuni ya mafunzo hayo ni kusambaza matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 na kuwajengea uwezo wadau wote wa namna ya kutumia matokeo hayo katika kutekeleza majukumu yao ya uongozi na utendaji serikalini na Mamlaka za Serikali za Mitaa, sekta binafsi ikiwemo biashara na uwekezaji, utafiti, utoaji huduma mbalimbali zikiwemo za kijamii na uchumi.

Alisema kufanya hivyo kutasaidia kuongeza uwazi na kupanua wigo wa matumizi ya matokeo ya sensa kwa serikali, sekta binafsi na wananchi kwa ujumla ili kupanga mipango jumuishi kwa maendeleo endelevu.

Katibu Tawala Mkoa wa Singida, Dk. Fatuma Mganga alisema mkoa huo umejipanga kuhakikisha mipango yao na programu zao zote za maendeleo zinapangwa kwa kuzingatia matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi, Sensa ya Majengo na Sensa ya Anwani za Makazi ya Mwaka 2022.

Alisema mbali ya kutekeleza maelekezo ya serikali, mkoa umeweka msisitizo wa matumizi ya matokeo ya sensa kwa lengo la kuhakikisha kuwa mipango na programu hizo zinajibu changamoto mbalimbali ambazo wananchi wanapambana nazo katika maisha yao ya kila siku.

# TASAF yashauriwa kufanyia kazi dosari kufikia malengo

**Na Paul Mabeja,** KONDOA

WADAU wa maendeleo wameshauri Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) katika Wilaya ya Kondoa mkoani kufanyia kazi dosari zilizopo ikiwamo ucheleweshaji wa malipo kwa walengwa, ili kusaidia kufikia lengo la kupunguza umaskini nchini.

Juzi, ubalozi wa Sweden, Uingereza, Ireland na Benki ya Dunia (WB) walitoa ushauri huo kwenye ziara ya kukagua na kufanya tathmini ya utekelezaji wa miradi ya TASAF katika Kijiji cha Itundwi na Bukulu wilayani humo.

Annie Homes kutoka ubalozi wa Uingereza nchini Tanzania alisema katika ziara hiyo wameona mambo mengi mazuri ambayo wanufaika wa mpango huo wamefanya katika kujikwamua kiuchumi.

"Katika ziara hii tumeona namna ambavyo walengwa wamefakiwa kupitia fedha za ruzuku ambazo wamekuwa wakipatiwa kujiongezea kipato kwa kuanza na kiasi kidogo cha fedha walinazopatiwa kufuga kuku, mbuzi na hatimaye wengine kununua ng'ombe.

"Tumeridhika na namna ambavyo miradi hii inavyotekelezwa lakini tunapendekeza kuwa TASAF kuongeza jitihada katika kusimamia walengwa wa mpango huu, lakini pia kuondoa dosari ambazo zimejitokeza ikiwemo ucheleweshaji wa malipo ya walengwa ili kusaidia kufikia malengo ya kupunguza umaskini Tanzania," alisema Homes.

Aidha, alisema kutokana na namna ambavyo walengwa wengi wameonekana na kunufaika na mpango huo ipo haja kuanza kutolewa elimu ili wahitimu na nafasi zao kuchukuliwa na watu wengine wenye uhitaji.

Naiseku Kisambu, kutoka ubalozi wa Sweden alisema pamoja na mafanikio waliyoyapa walengwa wa mpango huo wa kunusuru kaya maskini kupitia miradi mbalimbali bado ipo haja na kutilia mkazo suala la usawa wa kijinsia katika miradi ya TASAF.

Alisema bado lipo tatizo katika maeneo mengi katika suala la usawa wa kijinsia kwenye miradi ya TASAF, hali ambayo inapaswa kutiliwa mkazo ili kuongeza ushiriki wa makundi yote na kufikia azma ya kupunguza umaskini bila kumwacha mtu nyuma.

Mkurugenzi wa Uratibu TASAF makao makuu, Haika Shayo, alisema lengo la ziara hiyo ya siku tatu ni kufanya tathmini ya utekelezaji wa miradi kwa walengwa wa kaya maskini.

Shayo alisema: "Ziara kama hii pia inaendelea katika mikoa ya Mtwara, Kilimanjaro na Dodoma ambapo timu zetu zinatembelea utekelezaji wa miradi ya mpango wa ajira za muda na kusikiliza maoni yao namna ambavyo walivyonufaika na kubaini changamoto walizonazo na kuzitafutia suluhu".

Kadhalika, alisema ziara hiyo pia ina lengo la kuona namna ambavyo walengwa hao wamenufaika na mpango huo ili kuanza kuwaandaa ili wahitimu na kutoa nafasi kwa wengine.

"Elimu inahitajika hivi sasa kwa wanufaika wa mpango huu ambao wameonekana kujiongezea kipato ili waweze kuhitimu na kutoa fursa kwa wengine kuingia kwenye mpango," alisema.

Hata hivyo, alisema TASAF, itafanya tathmini ambayo itabainisha walengwa ambao wamejikwamua kiuchumi kwa kuanazisha miradi mbalimbali ili kuwaondoa kwenye mpango huo ili kuingiza watu wapya.

Alisema: "Tathmini iliyowahi kufanyika katika kipindi cha nyuma katika halmashauri 51 ilionyesha watu wapato 100 ndiyo walikuwa tayari kuhitimu kwa hiyari yao ili kupisha wengine kuchukua nafasi zao".





## Watumishi wa umma Mbeya watakiwa kujiendeleza kielimu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATUMISHI wa umma mkoani Mbeya, wametakiwa kutumia fursa ya uwepo wa vyuo mkoani humo kujiendeleza kielimu ili waongeze ujuzi na kuwatumikia wananchi vizuri.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa alitoa ushauri huo mwishoni mwa wiki wakati wa mahafari ya Chuo cha Maendeleo ya Jamii cha KAPS kilichopo Uyole jijini Mbeya.

Alisema serikali imetoa nafasi kwa watumishi wa kada mbalimbali kujiendeleza kielimu ili kuongeza tija katika kuwatumikia wananchi hasa katika ngazi za jamii.

"Nimefurahi hapa kati ya wanaohitimu pia wapo watendaji wa vijiji na kata ambao walikuwa wanajiendeleza, nitoe wito kwa watumishi wengine kutumia fursa ya uwepo wa vyuo hivi kujiendeleza kielimu," alisema Malisa.

Aliwataka wahitimu wa chuo hicho kwenda kuwatumikia wananchi bila kujali mazingira ya maeneo watakayopangiwa kwa maelezo kuwa wapo baadhi huwa wanataka kuajiriwa maeneo ya mjini pekee.

Aliwasisitiza kuyatumia maarifa waliyoyapata kulisaidia taifa hasa kwa kwenda kufanya kazi kwa bidii na kuhakikisha wanakuwa mabalozi wazuri wa maendeleo.

# YARA, MUST kushirikiana kuendeleza teknolojia kilimo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

KAMPUNI ya uzalishaji na usambazaji wa mbolea ya YARA Tanzania, imeingia makubaliano na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) kushirikiana, kuendeleza teknolojia za kilimo kwa lengo la kuongeza tija kwenye uzalishaji.

Aidha, taasisi hizo zimezindua kituo cha maarifa ya kilimo ambacho kitakuwa kinatumika kusambaza teknolojia za kilimo kwa wakulima, wataalamu wa kilimo pamoja na wajasiriamali wa mnyororo wa thamani wa mazao ya kilimo.

Makubalioano hayo yalifanyika mwishoni mwa wiki wakati wa uzinduzi wa kituo cha maarifa ambapo wadau mbalimbali walishiriki wakiwamo maofisa kutoka katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, wakulima, wajasiriamali wanaouza pembejeo za kilimo na wa mazao.

Bwanashamba Kiongozi wa Kampuni ya YARA anayesimamia Tanzania na Rwanda, Donath Fungu, alisema watakitumia kituo hicho kutoa elimu kwa wakulima kuhusu lishe kamili ya mazao, upimaji wa udongo pamoja na matumizi sahihi ya mbolea.

Alisema kampuni hiyo ina vituo nane Tanzania na Rwanda na kwamba kati ya vituo hivyo ni kimoja pekee ambacho kipo nchini Rwanda lakini vingine vyote vipo Tanzania.

Fungu alisema Kituo cha MUST kitatumika pia kutoa mafunzo ya kilimo kwa wanafunzi kutoka katika vyuo mbalimbali nchini ambavyo vinatoa elimu ya kilimo.

"Tunaandaa vituo vya maarifa ya kilimo katika mikoa mbalimbali kulingana na mazao yanayostawi katika mikoa husika, hiki hapa tutakitumia kufundishia kilimo cha mahindi, viazi mviringo na nyanya kwa sababu haya ndio mazao yanastawi zaidi huku," alisema Fungu.

Mtaalamu huyo wa kilimo alisema wataendelea kuongeza mazao ya kufundisha wakulima katika kituo hicho kadri muda utakavyokuwa unaenda kulingana na mahitaji na utafiti watakaoendelea kuufanya katika maeneo hayo.

Alisema lengo la kampuni hiyo ya YARA Tanzania ni kuongeza tija ya uzalishaji wa mazao mbalimbali ili kuinua uchumi pamoja na kuhakikisha kunakuwapo na uhakika wa chakula kwa taifa.

Makamu Mkuu wa Chuo cha MUST Taaluma, Prof. Godlivling Mtui, alisema waliingia makubaliano na YARA baada ya kuanzisha Ndaki ya Sayansi na Teknolojia ya Kilimo ambayo ni mpya chuoni hapo na inaendana na kile kinachofanywa na kampuni hiyo. Alisema chuo hicho kinafanya utafiti wa aina mbalimbali zinazohusu kilimo ikiwamo namna ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ambayo yanaikumba dunia kwa sasa na kutoa ushauri wa kitaalamu.

"Tutashirikiana kutoa elimu ya kitaalamu kwa wakulima, wenzetu YARA wako vizuri sana kwenye masuala ya mbolea na sisi ni wataalamu wa utafiti na teknolojia za kilimo kwa hiyo tunaamini ushirikiano huu utazaa matunda," alisema Prof. Mtui.

Katibu Tawala Msaidizi wa Uchumi na Uzalishaji wa Mkoa wa Mbeya, Said Maditto alipongeza Kampuni ya YARA Tanzania pamoja na Chuo cha MUST kwa kuanzisha kituo hicho kwa maelezo kuwa kitasaidia wakulima kuongeza tija.

Aliwataka wakulima wa Mkoa wa Mbeya kukitumia kituo hicho pamoja na vituo vingine vilivyoanzishwa na kampuni hiyo kujifunza teknolojia za kisasa za kilimo ili waongeze usalishaji wa mazao. Alisisitiza wakulima kupima afya ya udongo kwenye mashamba yao ili wafanye uchaguzi sahihi wa mazao yanayotakiwa kupandwa, aina ya mbegu zinazotakiwa kutumika pamoja na aina ya mbolea ya kutumia kwenye mashamba hayo.

"Tulishafanya utafiti kwenye zaidi ya vijiji 100 kwenye mkoa wetu na matokeo tulishayasambaza, ni wito wangu kwa wataalamu wa kilimo wa serikali na kampuni kushiriki kuwatafsiria wakulima matokeo yale na kuwashauri vizuri, lakini pia wakulima waje wajifunze hapa," alisema Maditto.

Alishauri wataalamu wa kilimo wa YARA kuweka vibao vyenye maelezo ya kitaalamu kuhusu uzalishaji wa mazao kwenye mashamba darasa yaliyopo kwenye kituo hicho ambacho kipo ndani ya Chuo cha MUST ili wakulima wajifunze kwa kusoma hata kama wataalamu hawapo.



Bwanashamba kiongozi wa kampuni ya uzalishaji na usambazaji wa mbolea ya YARA anayehudumia Tanzania na Rwanda, Donath Fungu, akitoa maelezo kuhusu kampuni hiyo wakati wa uzinduzi wa kituo cha maarifa ya kilimo kilichoanzishwa kwa ushirikiano kati ya kampuni hiyo na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# JKT Itende wafanya usafi Hospitali ya Kanda, watoa zawadi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MAOFISA wanawake wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) Kikosi cha 844 KJ Itende cha jijini Mbeya, wamefanya usafi wa mazingira katika Hospitali ya Kanda ya Mbeya Kitengo cha Wazazi Meta pamoja na kutoa zawadi kwa wanawake waliojifungua.

Maofisa hao walifanya matukio hayo juzi ikiwa ni mwendelezo wa maadhimisho ya miaka 60 tangu jeshi hilo lilipoasisiwa nchini ambapo pia waliwafariji wagonjwa waliolazwa kwenye hospitali hiyo.

Kiongozi wa msafara wa maofisa hao, Meja Goodluck Njau, alisema walianza maadhimisho hayo Julai mosi mwaka huu kwa kufanya shughuli mbalimbali za kijamii ikiwemo kufanya usafi wa mazingira katika maeneo mbalimbali.

Alisema waliamua kufanya usafi huo kwa lengo la kuwahamasisha wananchi kufanya usafi kwenye maeneo yao ili kuepuka magonjwa mbalimbali yanayotokana na uchafu. Alisema wakati maofisa wengine wakiendelea na shughuli zingine, umoja wa askari wanawake wa kikosi hicho walikwenda kufanya usafi kwenye Hospitali ya Meta na kuwafariji wanawake wenzao.

"Sisi tunaamini kwamba Hospitali ya Meta ndio chimbuko la taifa la kesho kwa maana kwamba hapa ndipo watoto wanapozaliwa, kwa hiyo askari wanawake wa kikosi chetu walikuja hapa kufanya usafi na kutoa zawadi kwa wenzao waliojifungua ili kutimiza malengo yetu tuliyojiwekea," alisema Meja Njau.

Alisema wataendelea kufanya shughuli mbalimbali za kijamii ndani ya mkoa huo katika kipindi chote cha maadhimisho ikiwa ni pamoja na malezi kwa vijana ikiwa ni sehemu ya kaulimbiu.

Mteule Daraja la Pili, Anna Nko alisema katika hospitali hiyo walifanya mazungumzo na kinamama waliojifungua kwa lengo la kuwapongeza na kuwatia moyo pamoja na kutoa zawadi mbalimbali.

Alisema walitoa zawadi kama mafuta ya kupakaa, sabuni na nguo kwa ajili ya kuwasitiri watoto na kwamba walichagua hospitali hiyo kwa sababu ndiyo inakusanya watu wengi zaidi.

"Tumefanya usafi lakini pia tumeongea na wanawake wenzetu kwa ajili ya kuwafariji na hatukuja mikono mitupu bali tulikuja na vitu vidogo ambavyo tumewagawia kama zawadi," alisema Afande Anna.

Nao baadhi ya vijana wanaopata mafunzo ya uzalishaji katika kikosi hicho walisema walishiriki kwenye shughuli hizo za kijamii ili kuiunga mkono serikali katika kuwahudumia wananchi.

Mmoja wa vijana hao, Irene Mushi alisema mbali na kufanya usfi na kutoa zawadi kwa wanawake katika hospitali hiyo, pia walifanya usafi katika Kituo cha Mabasi ya Chunya.

# ‘Elimu ya mnyororo wa thamani yahitajika kwa wavuvi’

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Maendeleo ya Uvuvi na Mazao ya Baharini, Dk. Salum Soud Hemed amesema elimu zaidi inahitajika ya kibiashara juu ya mnyororo wa thamani wa dagaa ili kupata maslahi mazuri kwa wajasiriamali wa uvuvi wa dagaa katika eneo la Fungurefu Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Aliyasema hayo wakati wa kikao na jumuiya za wajasiriamali waanika dagaa, wavuvi na wauzaji wa dagaa Zanzibar.

Dk. Salum alisema bidhaa ya dagaa imekuwa kubwa visiwani humo lakini hali bado hairidhishi kutokana na wajasiriamali kutokuwa kitu kimoja kupitia mnyororo wa thamani wa biashara hiyo.

Hivyo, aliwataka wajasiriamali hao kuwa na ushirikiano wa pamoja kati ya wavuvi, waanikaji na wasafirishaji wa bidhaa hiyo kwa lengo la kuzitatua changamoto zinazowakabili.

Aidha, aliwataka kuwa waaminifu katika utendaji wao wa biashara ya dagaa kutokana na Serikali ya Zanzibar kuwa na nia nzuri na wananchi wake katika kuleta maendeleo nchini.

Mkuu wa Divisheni ya Usarifu wa Mazao ya Bahari, Ali Khamis Shafi, alisema wapo tayari kusimamia usarifu wa dagaa ili kuondokana na changamoto zilizopo kwa lengo la kuinyanyua biashara hiyo kwa maslahi ya taifa.

# Bei ya petroli, dizeli Zanzibar yashuka

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

BEI ya mafuta ya petroli na dizeli kwa mwezi huu visiwani Zanzibar imeshuka kuliko sababishwa na kushuka kwa bei ya nishati hiyo katika soko la dunia.

Akitoa bei mpya za mafuta kwa waandishi wa habari Kaimu Kitengo cha Uhusiano wa Mamlaka ya Udhibiti wa Maji na Nishati Zanzibar (ZURA), Shara Chande, alisema licha ya kushuka kwa bidhaa hiyo katika soko la dunia lakini bado serikali inaendelea kufidia bei katika bidhaa zote za mafuta Zanzibar ili kuwapunguzia ukali wa maisha wananchi wake.

Alisema bidhaa ya nishati ni tegemezi zaidi katika harakati za kiuchumi kwa Zanzibar.

Kaimu huyo alisema mafuta ya petroli yatauzwa kwa Sh. 2,700 kutoka Sh. 2,730 ya mwezi uliopita, dizeli itauzwa kwa shilingi 2,746 kutoka shilingi 2,800, mafuta ya ndege yatauzwa kwa shilingi 2,190 kutoka shilingi 2,347 huku mafuta ya taa yakiendelea kubaki bei ya shilingi 2,921.

Alisema ZURA inapanga bei kwa kuzingatia mambo mbalimbali ikiwamo kubadilika kwa wastani wa bei za uuzaji wa bidhaa hizo katika soko la dunia pamoja na soko la ndani kupitia Bandari ya Dar es Salaam. Aidha, alisema pia ZURA inapanga bei kwa kuzingatia wastani wa mwenendo wa mabadiliko ya bei za mafuta duniani kwa mwezi uliopita ili kupata kianzio cha kufanyika mabadiliko ya bei za mafuta kwa mwezi huu.

Alisema jukumu lingine ni kuangalia gharama za uingizaji mafuta katika Bandari ya Dar es Salaam, kuangalia thamani ya shilingi dhidi ya dola, gharama za usafiri, bima hadi Zanzibar, kodi za serikali na kiwango cha faida kwa wauzaji wa jumla na rejareja.

Akizungumzia tathmini ya kuendelea kushuka kwa nishati hiyo miezi ijayo, Shara, alisema bado hawajajua kwa sababu kuna mambo ambayo yanasababisha kushuka au kupanda katika soko ikiwamo kupanda na kushuka kwa dola.

“Tunaweza leo mafuta yameshuka lakini kesho tukiamka mafuta yamepanda au pesa imepanda tunategemea na mambo yote ambayo tunayaweka hasa ukiangalia hatujaanza kushusha rasmi nishati hii moja kwa moja hapa Zanzibar bado tunaendelea kuchukua Tanzania Bara,” alisema. Alisema kushuka kwa nishati hiyo kwa kiasi kikubwa inaharakisha shughuli za kimaendeleo ikilinganishwa na miezi inayopanda ikiwamo kukua kwa shughuli za utalii na mataifa mbalimbali kusafiri zaidi hasa kuja Zanzibar.

Hata hivyo alisema ZURA inaendelea kufatilia na kudhibiti soko la mafuta na bei zake kwa ukaribu ikiwa ni pamoja na kuhakikisha bei za bidhaa hizo haziongezeki na kutokea athari katika shughuli za kijamii na kiuchumi.

Hivyo, aliwasisitiza wananchi kuwa bei hizo ndio bei halali na kuwahimiza kununua mafuta katika vituo vilivyokuwapo nchini na kudai risiti kila wanapopata huduma hiyo.



Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla, akitembelea mabanda ya wanaushirika na wajasiriamali wanaojihusisha na shughuli mbalimbali, alivutiwa na kazi zao kutokana na mwamko wao wa kujishughulisha ili kuongeza kipato binafsi na Taifa katika maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani yaliyofanyika Chuo cha Polisi Ziwani, Zanzibar. **PICHA: MPIGAPIGAPICHA WETU**

# Dk. Mwinyi avikumbusha majukumu vyama ushirika

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema vyama vya ushirika vina jukumu la kuwahamasisha, kuwaunganisha na kuwarahisishia wananchi ili washiriki katika harakati za kiuchumi, uzalishaji mali na utoaji huduma katika jamii.

Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, aliyasema hayo jana kwa niaba ya Rais Mwinyi katika Maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani.

Dk. Mwinyi alisema serikali inaendelea kufanya mageuzi makubwa ya vyama vya ushirika ikiwamo kuweka mazingira wezeshi ya sera, sheria na kanuni, hivyo ni wajibu wa vyama vya ushirika vinavyoanzishwa kuimarisha miamvuli yao ili uwasaidie kufanya na kuratibu shughuli zao kwa maslahi yao na taifa.

Alisema serikali itaendelea kusimamia na kuhakikisha misingi ya haki, uadilifu, demokrasia na utawala wa sheria vinaimarishwa katika vyama vya ushirika na kuboresha maslahi ya wanachama, kusimamia upatikanaji wa mitaji, mafunzo na masomo ili wanaushirika na wajasiriamali waweze kuzalisha bidhaa zenye viwango vya ushindani katika soko ambazo zitaleta fursa kubwa ya kukuza uchumi nchini.

Rais Dk. Mwinyi alizipongeza SACCOS nchini kwa kuhakikisha upatikanaji wa huduma za fedha hasa kwa wananchi wanaoishi vijijini na kueleza kuwa hatua hiyo ni kuunga mkono juhudi za serikali katika kuinua uchumi wa wananchi wake.

Kadhalika, alitoa wito kwa vijana wanaomaliza masomo katika ngazi tofauti watumie fursa ya kujiunga katika vyama vya ushirika ili kupeleka maarifa mapya na elimu waliyoipata katika masomo yao ili kuimarisha utendaji na kuchochea ufanisi katika vyama pamoja na kunufaika na ajira.

Aidha, alisema serikali kupitia Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) imeanzisha mafao ya upotevu wa ajira kwa lengo la kulinda na kumhifadhi mfanyakazi katika kukabiliana na ugumu wa maisha sambamba na kuwanufaisha wafanyakazi ambao wamepoteza ajira kuanzia Oktoba mwaka 2022.

Alisema serikali kwa kuwajali wananchi wake na kuwawezesha kiuchumi inajenga kiwanda cha kusarifu zao la mwani litakaposarifiwa Zanzibar litakalokuwa na bei nzuri itakayosaidia kuongeza kipato cha wakulima na wajasiriamali nchini.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudra Ramadhan Soraga, alisema kuwa wizara imeanza taratibu za kubadilisha sheria na kanuni za ushirika ambapo siku chache zijazo itaanza kushirikisha wadau vikiwamo vyama vya ushirika ili kutoa maoni yao na kupata sheria itakayosaidia kukuza sekta ya ushirika nchini.

Alisema tayari wizara kupitia Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi imeshasaini makubaliano na Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) kupunguza zaidi ya asilimia 95 za gharama za ubora wa viwango.

Katibu Mtendaji wa Muungano wa Vyama vya Ushirika Zanzibar (CUZA), Suleiman Ame Mbarouk, alisema kuwa sekta ya ushirika nchini inaendelea kukua siku hadi siku, kwamba hadi kufikia Juni 2023 Zanzibar vyama vya ushirika vilivyosajiliwa vimefikia 3,041 vyenye wanachama 51,656.

# Mwinyi ataka Afrika iongeze nguvu vita kuikabili rushwa

Na Allan Isack, ARUSHA

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amezitaka nchi za Afrika kupitia mamlaka zake za kupambana na rushwa kuungana katika mapambano ya kutokomeza rushwa.

Amesema rushwa ni chanzo cha kukwamisha shughuli za maendeleo miongoni mwa nchi nyingi za Afrika.

Alitoa rai hiyo jana jijini Arusha, alipowakilishwa na Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah, wakati wa ufunguzi wa mkutano wa maadhimisho ya Siku ya Kupambana na Rushwa Afrika.

Dk. Mwinyi alisema rushwa ina madhara makubwa ikiwamo kukwamisha shughuli za maendeleo hasa katika utekelezaji wa miradi na kwamba kuna umuhimu wa kupambana, kuzuia na kudhibiti kwa maslahi ya nchi hizo.

"Tushirikiane na kushikamana ili kuhakikisha kuwa tunadhibiti rushwa kwa kuwa ni adui wa haki na maendeleo kwa nchi zetu," alisema Dk. Mwinyi.

Kadhalika, alitoa rai kwa wananchi kuwa mabalozi wema wa kutoa elimu na taarifa ili Afrika ifanikiwe kwenye suala la mapambano dhidi ya rushwa.

Alisema katika kuonyesha dhamira ya dhati ya mapambano hayo, Tanzania ilikuwa miongoni mwa nchi zilizoridhia Mkataba wa Mapambano Dhidi ya Rushwa mwaka 2003.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Salum Hamduni, alisema ufunguzi wa maadhimisho hayo yatakuwa kwa siku tatu na kutakuwapo kwa washiriki zaidi ya 700 kutoka nchi mbalimbali za Afrika.

Alisema katika maadhimisho hayo pia kutafanyika matembezi ya kupinga rushwa, maonyesho kwenye mabanda ikiwamo kutoa elimu ya masuala ya rushwa, elimu ya dawa za kulevya, kongamano na kilele cha maadhimisho.

Kadhalika, alisema siku ya kilele wanatarajia mgeni rasmi atakuwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Naye Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, alisema kwenye maadhimisho hayo taasisi 33 kutoka ndani na nje ya Tanzania zimethibitisha kushiriki.

"Tanzania tuna dhamira ya kupambana na rushwa na tuko tayari kushirikiana na washirika wetu kupiga vita rushwa," alisema Simbachawene.

Kadhalika, alisema kwenye mkutano huo mamlaka za kuzuia na kupambana na rushwa zitapata fursa ya kubadilishana uzoefu wa utendaji kazi.

Maadhimisho ya Siku ya Mapambano ya Rushwa Barani Afrika yameanza Arusha na kaulimbiu ni: 'Mafanikio ya miaka 20 ya Umoja wa Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa'.




Mkuu wa Kitengo cha Rasilimali Watu wa Benki ya Absa, Patrick Foya, akizungumza wakati wa hafla ya uzinduzi wa lengo jipya la benki hiyo liitwalo 'Tunaiwezesha Afrika ya kesho pamoja, hatua moja baada ya nyengine' jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwanafunzi auawa wezi wakitaka fedha alizolipwa TASAF

Na Said Hamdani, LINDI

MWANAFUNZI wa kidato cha tatu, Shule ya Sekondari Ally Mchumo, Tarafa ya Kipatimu, mkoani Lindi, Jamila Adamu (17), ameuawa kwa kuchomwa na kitu chenye ncha kali na watu waliovamia nyumba yao wakitaka wapewe fedha walizopokea kutoka Mfuko Maendeleo ya Jamii (TASAF).

Kwa mujibu wa taarifa zilizothibitishwa na viongozi wa Serikali ya Kijiji, Kata na Kamanda wa Polisi mkoani hapa, tukio hilo lilitokea Juni 30, mwaka huu.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Chumo, Abdallah Ngomba, alisema, tukio hilo lilitokea baada ya vijana wawili kuvamia nyumbani kwa mama wa marehemu Jamila, Manate Kikaka na kulazimisha wapewe fedha alizolipwa na TASAF.

Alisema siku ya tukio, Jamila na mama yake wakiwa ndani ya nyumba yao wamelala, vijana wawili aliowataja kwa majina, Nassoro Mailo na Abbasi Kapandaila, waliingia ndani mwao na kuanza kupekua wakitafuta fedha ndipo Jamila aliposhtuka kutoka usingizini na kupiga kelele za wezi.

Ngomba alisema kitendo cha kupiga kelele za kuomba msaada huo, vijana hao waliokuwa na silaha zenye ncha kali walimchoma mwanafunzi huyo kwenye mbavu na kutokomea zao kusikojulikana.

"Wakati wakipekua mule ndani, Jamila aliamka na kuuliza nyie kina nani? Wakamwambia awape fedha alizolipwa na TASAF," alisema Ngomba.

Ofisa Mtendaji Kata ya Chumo, Marachius Mutalemwa, amekiri kutokea kwa tukio hilo na kwamba watuhumiwa wote wawili wamekamatwa na kufikishwa kituo cha polisi, mji mdogo Masoko, Wilaya ya Kilwa wakiendelea kuhojiwa.

Mutalemwa alisema hilo ni tukio la pili kufanywa na watuhumiwa hao, kwa kuwa wiki mbili zilizopita wanadaiwa kuiba Sh. 80,000 kwa wazee wengine waliokuwa wamelipwa fedha zinazotokana na TASAF.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, ACP Pilli Mande, amekiri kutokea kwa mauaji hayo na kueleza tayari vijana wawili wanaodaiwa kuhusika na mauaji ya mwanafunzi huyo wanawashikilia kwa mahojiano.

Mande alisema watuhumiwa wote kwa pamoja wanatarajia kufikishwa mahakamani baada ya kukamilisha kazi ya upelelezi wa tukio hilo.

# Katambi atoa siku 14 kiwanda kuboresha mazingira

Na Frank Monyo

NAIBU Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Patrobas Katambi, ametoa siku 14 kwa uongozi wa kiwanda cha Colourful Industry Limited kilichopo Buza-Temeke, jijini Dar es Salaam kuboresha mazingira ya kazi pamoja na kushughulikia changamoto mbalimbali za wafanyakazi.

Alitoa kauli hiyo jana alipofanya ziara katika viwanda vya Mkoa wa Dar es Salaam na kuelezwa kutoridhishwa na hali ya utekelezaji wa Sheria za Kazi, Usalama na afya pamoja na hifadhi kwa jamii katika baadhi ya viwanda.

Akizungumza baada ya kufanya ukaguzi wa mifumo ya usalama na afya na uzingatiaji wa sheria za kazi katika kiwanda hicho alisema..."nimetembelea sehemu mbalimbali za uzalishaji katika kiwanda hiki na kubaini ukiukwaji mkubwa wa taratibu za usalama na afya mahali pa ikiwamo wafanyakazi kutopatiwa vifaa vya kujikinga na vihatarishi vya magonjwa na ajali.

Hali ya mazingira ya kazi siyo nzuri kuna mzunguko finyu wa hewa na hata mwanga hautoshelezi," alisema Katambi na kuongeza:

"Aidha kuna ukiukwaji wa haki nyingine za wafanyakazi ikiwamo ujira mdogo, wafanyakazi kulazimishwa kufanya kazi kwa zaidi ya saa zinazoruhusiwa kisheria bila kupatiwa malipo ya ziada pamoja na kutowasilisha michango ya wafanyakazi katika mifuko ya hifadhi kwa jamii," alisema.

Pia, alitembelea Kiwanda cha Steel Masters Limited kilichopo Chang'ombe, jijini Dar es Salaam kinachozalishaji bidhaa za chuma na kufanya ukaguzi wa maeneo ya uzalishaji pamoja na masuala mengine yanayohusu utekelezaji wa sheria za kazi, usalama na afya na hifadhi kwa jamii. Akiwa katika kiwanda hicho, alibaini upungufu katika utekelezaji wa sheria tajwa ikiwamo wafanyakazi kutokingwa na kilele zinazalishwa na mitambo pamoja na taarifa zisizojitosheleza kuhusu uwasilishwaji wa michango katika mifuko ya hifadhi kwa jamii.

Aliwaagiza maofisa kutoka Taasisi chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu kurudi tena katika kiwanda hicho kwa ukaguzi zaidi na kushauri namna bora zaidi itakayowezesha kiwanda hicho kutekeleza sheria za kazi, usalama na afya pamoja na hifadhi kwa jamii.

Mwakilishi wa Kampuni ya Steel Masters Limited, Gajendra Narendra, alimshukuru Naibu Waziri kwa kufanya ziara katika kiwanda chao na kutoa ushauri na maelekezo mbalimbali.

"Tupo tayari kuyafanyia kazi maelekezo yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri, tunamuahidi kwamba tutayafanyia kazi kwa mwongozo wa wataalamu wake na tupo tayari kumwalika tena baada ya kukamilisha maboresho hayo," alisema Narendra.




Ofisa Mkuu wa Biashara wa Benki ya CRDB, Boma Raballa (wa pili kulia) na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania, Nyakaho Mahemba (wa pili kushoto), wakitia saini mkataba wa ushirikiano wa kutoa huduma za fedha kwa wadau wa mfuko wa utamaduni na sanaa jijini Dar es Salaam juzi. Kulia ni Mkuu wa Kitengo cha Sheria Benki ya CRDB, Pascal Mihayo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CRDB kutoa mikopo nafuu kwa wasanii

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya miezi sita ya uzoefu wa Mfuko wa Utamaduni na Sanaa kutoa mikopo kwa wasanii nchini, sasa umeingia mkataba na Benki ya CRDB kutanua wigo wa fursa hizo ili ziwanufaishe wananchi wengi zaidi kupitia mtandao wake mpana wa matawi na mawakala.

Mpaka sasa, mfuko huo ulioinduliwa Desemba 2022 umeshakopesha Sh. bilioni 1.077 kwa miradi 45 ikiwamo 29 inayomilikiwa na kuendeshwa na wanaume, 12 ya wanawake na kikundi kimoja.

Katika hafla ya kuingia makubaliano ya mkataba huo, Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Pindi Chana, alisema jijini Dar es Salaam juzi kwa muda mfupi ambao mfuko huo umetoa fedha hizo, serikali imeona mahitaji makubwa yaliyopo, hivyo kuamua kuipeleka jirani na wananchi.

"Benki ya CRDB ina matawi nchini kote. Tunataka mikopo hii ipatikane kila mahali alipo msanii ili kukuza kipaji chake kwa kuwa sasa hivi jamii imeiona faida ya sanaa na wazazi wengi wapo tayari kuwapa rukhsa watoto wao kuingia kwenye usanii.

"Kwa mikopo hii kupatikana kwenye matawi ya benki, itawapunguzia wanufaika gharama za kuifuata Dar es Salaam," alisema Waziri Pindi.

Mbali na kuwapa mikopo, waziri alisema wizara pia imeanza kuwatafutia wasanii fursa za nje ya nchi ambako wanashiriki matamasha hayo wanajiongezea mtandao wa washirika, hivyo kutanua fursa za kipato zaidi.

"Mikopo hii itapatikana kwa riba ya asilimia tisa tu. Hiki ni kiwango cha chini kulinganishwa na riba zilizopo sokoni kwa sababu serikali imeweka mkono wake. Ninawasihi wasanii popote walipo nchini wajitokeze kunufaika na fursa hii," alisisitiza waziri huyo.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini wa Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania, Abdulmajid Nsekela, alisema wanafanya kila wawezalo kuinua ubora wa kazi za utamaduni na sanaa ili kujiendesha kibiashara na kutengeneza ajira nyingi kwa vijana nchini kwa kuwapa mikopo na mafunzo tangu uliposajiliwa mwaka 2020.

"Kati ya mikopo tuliyoitoa, wanaume wamepokea Sh. milioni 737 huku wanawake wakichukua Sh. milioni 275. Kikundi kimoja kilichojitokeza kimekopeshwa Sh. milioni 10 pamoja na kampuni tatu zilizowezeshwa Sh. milioni 55.

"Kiwango cha marejesho kinaridhisha kwani ni asilimia 88 na tutazidi kusimamia ipasavyo ili kifikie asilimia 95 inayotakiwa," alisema Nsekela.

Ili kuwawezesha wanufaika kuzitumia fedha za mikopo inayotolewa kwa malengo yaliyokusudiwa, Nsekela alisema mfuko umetoa mafunzo kwa wadau 7,216 katika mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Dodoma, Kilimanjaro, Morogoro, Tanga na Pwani na kufanikisha uanzishwaji wa vitendea kazi kwa vyuo vitano ambavyo ni Simba Scratch Academy, Koshuma Training Institute, Mwanamboka Ujuzi-Hub, Dage School of Dressing na AM Fashion.

"Ninaomba kuwafahamisha wadau kuwa, mpango huu utakaoushuhudia leo utakuwa suluhisho la changamoto zilizokuwa zinawakumbuka wasanii, hivyo nitaomba tuuamini, tuupokee na kutoa ushirikiano ili kutimiza ndoto za Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan," alisema Nsekela ambaye pia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB.

Akitia saini mkataba huo, Ofisa Mkuu wa Biashara wa Benki ya CRDB, Boma Raballa, alisema ni siku ya kihistoria kuona mkakati wa unatafsiriwa kwa vitendo kwa kuishirikisha sekta binafsi ili kuwafikia wasanii wengi.

"Benki ya CRDB imeingia katika mpango huu kuhakikisha malengo ya mfuko yanafikiwa. Tuna imani kuwa kwa kushirikiana na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, pamoja na taasisi za serikali, tutafanikisha kuyafikia malengo ya mfuko huu.

"Tumekuwa tukiona jitihada za serikali kujenga mazingira rafiki kwa wadau wa utamaduni, sanaa na michezo ili kuwawezesha kupata matunda ya kazi zao kupitia vipaji walivyonavyo kwa manufaa yao binafsi, familia zao hata jamii na Taifa kwa ujumla," alisema Raballa.

Ili msanii apate mkopo ambao ni kuanzia Sh. 200,000 mpaka Sh. milioni 100, Raballa alisema atatakiwa kupeleka maombi yake ofisi za mfuko huo zinazopatikana nchi nzima ili kufanya uhakiki wa awali kisha kupendekeza maombi hayo yaende Benki ya CRDB. Maombi yakikidhi vigezo, mfuko utalipeleka tawi la Benki ya CRDB lililo jirani na msanii husika.

# WMA yawapa siri wanunuzi petroli, dizeli

**Na Joseph Mwendapole**

WAKALA wa Vipimo (WMA), imewataka wanunuzi wa petroli na dizeli kununua mafuta hayo kwenye pampu zilizowekwa stika za WMA pekee ili kuepuka kupunjwa mafuta.

Pia, imewataka wamiliki wa vituo vya mafuta kuhakikisha pampu wanazotumia zimewekewa stika za wakala kuonyesha kwamba zimehakikiwa na wakala kuepuka kuwapunja wateja.

Wito huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa WMA, Stela Kahwa, wakati akizungumza kwenye Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa yanayoendelea kwenye viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere, Temeke, jijini Dar es Salaam.

Alisema WMA ilifanya ukaguzi na kuzihakiki pampu zinazotumiwa kupimia petroli na dizeli kama mkakati wa kuhakikisha mtumiaji wa mafuta hayo hapunjwi kipimo.

"Mnunuzi wa mafuta anapaswa kuangalia stika ya WMA kama haipo hiyo mita haijakaguliwa wala kuhakikiwa kwa hiyo ukiona hivyo hamia kwenye pampu nyingine au kituo kingine kwasababu sisi tunataka ukitoa hela yako basi upate thamani ya hela yako usipunjwe," alisema.

Alisema wakala imejitahidi kukagua vituo vyote nchi nzima na wafanyabiashara wengi wa mafuta wanajua kuhusu utaratibu huo na wengi wameweka stika zinazoonyesha wamekaguliwa na kuhakikiwa vituo vyao.

Alisema hata mizani ambayo inapima bidhaa za madukani imekaguliwa na kuwekewa stika za WMA na kwamba ni wajibu wa wananchi wanapopimiwa kuhakiki kama mizani imewekewa stika kuepuka kupunjwa.

Alisema wanawasaidia wajasiriamali wadogo wakue na kupenya kwenye masoko ya kimataifa kwa kuwaelekeza namna bora ya kufungasha bidhaa zao kisasa.

"Ukikosea kwenye kufungasha na kuweka lebo inamaana bidhaa zako zinaweza kukataliwa kwenye soko la kimataifa au hata kwenye masoko ya ndani na ya Afrika Mashariki, ndiyo maana tunawatembelea na kuwapa elimu," alisema.

Aidha, alisema baada ya mafunzo hayo wafanyabiashara wengi wadogo waliofika kwenye maonyesho ya mwaka huu, wameonyesha mafanikio makubwa kulinganisha na miaka iliyopita.

"Elimu hii huwa tunawapa bure na wenyewe wamekiri kwamba imewasaidia kupenya kwenye masoko ya nje na hata eneo la ufungashaji, ukiwatembelea kwenye maonyesho haya unaona kabisa namna walivyoboresha biashara zao," alisema.

Alisema WMA ni mwanachama wa Shirikisho la Vipimo Duniani na inawajibika kusimamia vipimo kwa bidhaa zote zinazozalishwa nchini na zinazoingizwa kutoka nje ya nchi.

Alisema ili bidhaa zinazozalishwa nchini ziweze kupata masoko makubwa ya kimataifa, zinalazimika kufuata viwango na maelekezo ya mashirika ya kimataifa ulimwenguni.

"Tunasimamia biashara kwa maana ya afya usalama na mazingira, watu wametuzoea kwamba sisi tunasimamia mizani kwenye bucha na mizani kwenye maduka lakini sisi tunasimamia vipimo vyote vinavyotumika kwenye biashara kuhusu uzito na urefu," alisema.

Alisema wameingia kwenye upimaji wa gesi asilia, mita za maji na umeme na sasa wanaelekea kwenye kupima viwango vya sauti na kelele zinazolalamikiwa kwenye kumbi za starehe ili kuwe na viwango vinavyokubalika.

"Tumewasikia wenzetu Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kwamba kuna sehemu za starehe zinapiga muziki kwa sauti kubwa na kusumbua majirani wa maeneo hayo kwa hiyo na huko tumeingia kupima sauti ili kuondoa malalamiko," alisema.

Alisema WMA ni rafiki wa walaji na wafanyabiashara na ndiyo sababu imekuwa ikisimama katikati kuhakikisha biashara inafanyika kwa haki na kila mmoja anapata anachostahili na kuondoa malalamiko.

HABARI MICHEZO

# SIMBA KUMPELEKA KYOMBO SINGIDA FG IKIMULIKA COASTAL

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kumpeleka kwa mkopo beki wake wa kati raia wa Kenya, Joash Onyango, katika Klabu ya Singida Fountain Gate, Simba ipo mbioni kumtoa pia straika wake mzawa Habib Kyombo.

Habari kutoka ndani ya Klabu ya Simba, zimeeleza kuwa Kyombo naye huenda akapelekwa kwa mkopo baada ya kukosa namba kwenye kikosi cha kwanza, huku msimu ujao ikitabiriwa kuwa na ushindani zaidi.

Wakati ikiwa mbioni kufanya hivyo, klabu inakaribia kukamilisha usajili wa mchezaji wa Kitanzania, Mtenje Albano kutoka Coastal Union.

"Tunataka kurekebisha kikosi chetu badala ya kuwa na wachezaji wa akiba ambao wapo tu, ili kuingia wakati wenzao wamechoka. Tunataka kuwa na wachezaji ambao wakiingia watakuwa kama wale waliotoka au zaidi, na kikubwa ni wale wataokuwa wakienda kubadilisha matokeo, au kuzidi kuwaharibu wapinzani.

"Hicho ndicho tunachotaka kufanya msimu huu, kwa hiyo wale ambao hata kwenye kikosi cha msimu uliopita walikuwa na changamoto ya kupata namba, watatusamehe msimu huu," kilisema chanzo ndani ya klabu hiyo kilichofichua kutolewa kwa Kyombo kwa mkopo.

Mchezaji huyo alijiunga na Simba mwanzoni mwa msimu uliopita akitokea Mbeya Kwanza na alitarajiwa angekuwa mrithi wa John Bocco ambaye umri unaanza kumtupa mkono, lakini haikuwa hivyo.

Aidha, chanzo chetu hicho kilieleza kuwa Mtenje atasajiliwa kwenda kuongeza ushindani wa namba kwenye nafasi ya kiungo mkabaji, ili kuwa na watu wanne kwenye eneo hilo, Sadio Kanoute, Mzamiru Yassin, na mchezaji mwingine atakayesajiliwa kutoka nje ya nchi.

Kama dili hilo likikamilika, huenda Mtenje akawa mchezaji wa kwanza mzawa msimu huu kusajiliwa na klabu hiyo.

Kiungo huyo mkakamavu aliingia matatani na kutolewa nje kwa kadi nyekundu alipomchezea rafu, Yannick Bangala kwenye moja kati ya mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara msimu uliomalizika.

NGOMA...




Wasanii wa Kikundi cha Ngoma za Asili cha Elimisha Group, wakicheza ngoma ya Kizaramo katika viwanja vya biashara Sabasaba, Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Moalin anukia kuibukia KMC FC

**Na Saada Akida**

KLABU ya KMC yenye maskani yake Kinondoni, Dar es Salaam, iko katika hatua za mwisho kumalizana na aliyekuwa Kocha wa Azam FC, Abdihamid Moalin, kwa ajili ya kukinoa kikosi chao kuelekea msimu wa 2023/24.

Moalin aliyefundisha Azam FC msimu uliopita kabla ya kuondolewa baada ya kutofikia malengo ya timu hiyo kwa sasa anahusishwa kupewa kuinoa KMC FC.

Katikati ya msimu wa 2022/23, KMC ilimfuata kazi kocha wao, Thierry Hitimana na kumkabidhi mikoba Jamhuri Kihwelo (Julio), akitakiwa kuhakikisha inaibakisha timu hiyo Ligi Kuu Bara, malengo ambayo alifanikiwa kuyatimiza baada ya kuponea kwenye 'Play Off' dhidi ya Mbeya City itakayoshiriki Championship msimu ujao.

Akizungumza na Nipashe jana, Mtendaji Mkuu wa KMC FC, Daniel Mwakasungula, alisema wanaendelea kufanya maboresho makubwa ndani ya timu yao na suala la mabadiliko ya benchi la ufundi yapo kwenye ngazi ya juu.

Alisema suala la benchi la ufundi ni mapema kulizungumzia kwa sababu leo bodi ya wakurugenzi ya timu hiyo inatarajiwa kukutana kwa ajili ya mrejesho wa kikao cha kwanza kilichofanyika mapema baada ya kutamatika kwa msimu wa 2022/23.

"Kutakuwa na maboresho katika timu ikiwamo usajili ambao tayari tumeshamaliza kwa kuwaongezea mikataba baadhi ya wachezaji wetu na kuwasajili wale waliopendekezwa katika ripoti ya makocha waliokuwapo.

"Siwezi kuzungumzia juu ya kocha Moalin kwa sababu hilo lipo ya juu ya uwezo wangu, hivi sasa liko katika ngazi ya juu kama bodi watalileta huku kwetu basi tutalitolea ufafanuzi," alisema Mwakasungula.

Alisema katika usajili wamejipanga vizuri kwa kusajili kulingana na mahitaji ya msimu ujao pamoja na kufanya maboresho mengine ya miundombinu ikiwamo suala la usafiri ambalo lilikuwa changamoto kwa wachezaji wao.

"Awali, tulikuwa na basi dogo ambalo wachezaji walilalamika linawasababishia majeraha hasa wanapokuwa kwenye safari ndefu, tayari limefanyiwa," alisema na kuongeza:

"Suala la kambi ndani ya wiki hii tutaweka wazi ni lini tunaingia kambini na wapi tutakapoiweka kuanza rasmi maandalizi ya msimu mpya wa ligi," alisema mtendaji huyo.

# JKT kutekeleza agizo la Mama

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

WAZIRI wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Innocent Bashungwa, amesema wataendelea kutekeleza agizo la Rais Samia Suluhu Hassan la kuboresha miundombinu ili kuibua vipaji vya wanamichezo chipukizi.

Bashungwa aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari katika kilele cha maadhimisho ya miaka 60 ya jeshi hilo tangu lianzishwe, yanayotarajia kufanyika leo kwenye viwanja vya Jamhuri jijini Dodoma.

Alisema Jeshi hilo linashiriki michezo mbalimbali ya kitaifa na kimataifa, hivyo katika maadhimisho hayo kutakuwa na wasanii ambao watatoa burudani kwa Watanzania watakaojitokeza katika kilele hicho.

"Jeshi hatushindwi kufanya chochote, kila timu yetu kwenye mashindano yoyote, lazima ifanye vizuri, tunaendelea kuboresha timu za michezo mbalimbali ili zishiriki michezo ya kimataifa," alisema Bashungwa.

Alisema lengo lao ni kuona timu za jeshi hilo zinafanya vizuri kwenye mashindano mbalimbali ya michezo ya kitaifa na kimataifa, huku akitolea mfano kwenye michezo ya riadha, ngumi na soka la wanawake ambayo wamekuwa wakifanya vizuri.

Waziri Bashungwa alizipongeza pia timu za soka za Veterani JKT na Twalipo baada ya kutoka sare ya kufungana mabao 2-2, katika bonanza la mchezo wa kuadhimisha miaka 60 ya jeshi hilo.

Kwa upande wa Katibu wa Kamati Ndogo ya maadhimisho hayo, Kapteni Godwin Ekingo, alisema lengo la mashindano hayo ni mbali ya kusherehekea miaka 60 ya jeshi hilo, lakini ni kuonyesha vitu mbalimbali ambavyo wanavifanya ukiacha kulinda taifa.

"Tumeandaa bonanza la michezo mbalimbali ikiwamo soka, mpira wa kikapu, mpira wa wavu na netiboli, hii yote ni kutaka kuonyesha JKT ni sehemu ya jamii," alisema Kapteni Ekingo.

Naye Kanali Juma Mray, alisema ukiacha bonanza hilo, wamefanya pia michezo mingine kama JKT Marathon ambayo ilijumuisha wanariadha kutoka sehemu mbalimbali hapa nchini.

Kwa upande wa mchezaji wa zamani wa Simba na Timu ya Taifa, 'Taifa Stars', Lubigisa Madata, aliipongeza JKT huku akisisitiza bonanza kama hilo linachangia kuibua vipaji vya wachezaji chipukizi.

Aidha, alizitaka taasisi nyingine kuiga mfano wa JKT kuandaa bonanza ambalo litasaidia kuibua vipaji vya wachezaji chipukizi.

## ZISIKUPITE

### KANE NA OFA MPYA

KLABU ya Bayern Munich inatarajiwa kutoa ofa nzuri zaidi yenye thamani ya karibu pauni milioni 70 kwa ajili ya mshambuliaji wa England, Harry Kane lakini ofa hiyo haifiki kiwango kinachotakiwa na Tottenham Hotspur, licha ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, kusaliwa na mwaka mmoja kwenye mkataba wake. **(Mail on Sunday)**

### CHELSEA NA DAU LA LUKAKU

CHELSEA inataka pauni milioni 40 kwa anayetaka kumnunua mshambuliaji wa Ubelgiji, Romelu Lukaku, ambaye anazivutia klabu za Al-Hilal na Juventus, wakati Inter Milan wamekataliwa ofa yao waliyotoa awali kwa ajili ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30. **(Guardian)**

### HOJLUND AWINDWA UNITED

KLABU ya Manchester United imekubaliana masharti binafsi na mshambuliaji wa Denmark, Rasmus Hojlund, na yuko tayari kuiomba Atalanta kumruhusu kuondoka ikiwa klabu hiyo ya Old Trafford haitawezi kuafikiana na miamba hiyo ya Italia, ambayo inataka pauni milioni 60 kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20. **(Football transfers)**

### CUCURELLA ATAKIWA SPURs

TOTTENHAM Hotspur inamfuatilia, Marc Cucurella mwenye umri wa miaka 24, ambaye anaweza kucheza kama beki wa kushoto au winga wa upande huo, wakati huu wakitafuta mbadala wa winga wao raia wa Croatia, Ivan Perisic, 34. **(Football Transfers)**

### ITAKURA AFUATILIWA SPURS

KLABU za Tottenham Hotspur na Napoli zinawania kumsajili beki wa Borussia Monchengladbach na Japan, Ko Itakura, 26. **(Sky Sports Germany, via Get German Football News)**

### MBAPPE ALALAMIKIWA PSG

WACHEZAJI sita wa Paris Saint-Germain, wakiwamo wawili waliosajiliwa majira ya joto wamelalamikia uongozi kuhusu maoni yaliyotolewa na mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe, 24. **(Sky Sports)**

### CHELSEA KWA BALOGUM

KLABU ya Chelsea imeanza mazungumzo na Arsenal kuhusu mpango wa kumnunua mshambuliaji wa Marekani, Folarin Balogun, 22. **(Mail on Sunday)**

### ZAHA ASIKILIZIA OFA

WINGA wa Ivory Coast, Wilfried Zaha, ambaye mkataba wake unamalizika pale Crystal Palace, anatathmini ofa mpya, wakati mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, pia amefanya mazungumzo na PSG, Napoli na Galatasaray. **(Mail)**

### PELLISTRI ATAKIWA TWENTE

KLABU ya FC Twente ya Uholanzi inamtaka kwa mkopo mshambuliaji wa Manchester United na Uruguay, Facundo Pellistri, 21. **(Voetbal International)**

### BAYERN YAMTAKA MIN-JAE

KLABU ya Bayern Munich inataka kumsajili kwa euro milioni 50 beki wa Napoli, Kim Min-jae na watamsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 kwa mkataba wa miaka mitano hadi 2028. **(Sky Sports Germany)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# DE GEA ASHUSHA UJUMBE MZITO AKIAGA MAN UNITED

●●●Manchester daima itakuwa moyoni mwangu, imenitengeneza na haitawahi...

**MANCHESTER, England**

DAVID de Gea ametangaza kuondoka Manchester United msimu huu wa majira ya joto na amesema kuwa sasa ni wakati muafaka wa kutafuta changamoto mpya katika maisha yake ya soka.

Golikipa huyo alishindwa kuafikiana kuhusu mkataba mpya wa kuongeza muda wake pale Old Trafford na ataondoka katika klabu hiyo baada ya kukaa kwa miaka 12 tangu alipojiunga nayo akitokea Atletico Madrid mwaka 2011.

De Gea alikuwa karibu kusaini mkataba mpya, baada ya mazungumzo kuvunjika mwishoni mwa msimu. Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba United iko kwenye mazungumzo na Inter Milan kwa ajili ya uhamisho wa mlinda mlango wa Cameroon, Andre Onana.

"Nilitaka tu kutuma ujumbe huu wa kuwaaga mashabiki wote wa Manchester United," De Gea aliandika kwenye mtandao wa kijamii.

David de Gea alicheza mechi 545 akiwa na Manchester United katika kipindi cha miaka 12 katika klabu hiyo.

"Ningependa kutoa shukrani zangu zisizo na shaka na shukrani kwa upendo wa miaka 12 iliyopita. Tumefanikiwa mengi tangu mpendwa wangu Sir Alex Ferguson aliponileta katika klabu hii.

"Nilijivunia sana kila nilipovaa jezi hii, kuiongoza timu, kuwakilisha taasisi hii, klabu kubwa zaidi duniani ilikuwa ni heshima iliyotolewa kwa wanasoka wachache waliobahatika.

"Kimekuwa kipindi kisichosahaulika na chenye mafanikio tangu nilipokuja hapa. Sikufikiria kutoka Madrid nikiwa kijana mdogo, tungefanikisha tulichofanya pamoja.

"Sasa, ni wakati muafaka wa kuchukua changamoto mpya, kujisukuma tena katika mazingira mapya.

"Manchester daima itakuwa moyoni mwangu, imenitengeneza na haitawahi kuniacha. Tumeyaona yote."

De Gea alicheza mechi 545 akiwa na United na kuwa nafasi ya saba kwenye orodha ya wachezaji waloichezea klabu hiyo kwa muda mrefu zaidi.

Alikuwa sehemu ya timu iliyoshinda taji la Ligi Kuu England msimu wa chini ya Sir Alex Ferguson. Pia alishinda Kombe la FA mwaka 2016, Kombe la Carabao mnamo 2017 na 2023 na Ligi ya Europa mwaka 2017.

Katika taarifa ya klabu iliyotolewa muda mfupi baada ya kutangazwa kwa De Gea, kocha Erik ten Hag alisema: "Inahitaji ubora na tabia kubwa kufikia kiwango chake.

"Kucheza mara 545 katika kipindi cha miaka 12 ni mafanikio ya pekee, hasa katika nafasi ya golikipa ambapo kila mchezo unakuweka kwenye nafasi ya uangalizi. Kuwa mshindi wa tuzo za mchezaji bora wa mwaka kutoka kwa mashabiki na wachezaji wenzake, kila mmoja kwa mara nne, inaonesha kiwango cha uchezaji wake na atakumbukwa daima kama mmoja wa makipa bora kabisa katika historia ya klabu."

## HABARI MICHEZO



# RICHARLISON AMTOLEA POVU CONTE

**LONDON, England**

MSHAMBULIAJI wa Tottenham Hotspur, Richarlison, amesema kocha wa zamani, Antonio Conte, alimfokea kwa takriban saa mbili katika mkutano wa timu.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil alivumilia msimu ngumu wa kwanza katika Klabu ya Spurs msimu uliopita chini ya Conte kabla ya Muitaliano huyo kutimuliwa na klabu hiyo Machi mwaka huu.

Richarlison alikuwa amemkosoa Conte kufuatia kuondolewa kwa Tottenham kutoka hatua ya 16 bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kabla ya timu hiyo kujibu na kumweleza mchezaji huyo kuwa "mbinafsi."

Richarlison alisema alikosea kumkosoa kocha wake hadharani na akapokea adhabu yake mbele ya wachezaji wenzake.

"Ni kweli nilijifanya mjinga kwa kusema kwenye mahojiano kwamba nahitaji muda na kila kitu kingine, ilikuwa baada ya kuondolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini nilimwomba msamaha," alisema Richarlison.

Conte alimsajili Richarlison kutoka Everton mwanzoni mwa msimu wa 2022-23, lakini mshambuliaji huyo alikuwa na wakati mgumu kutokana na majeraha.

# Man City yapambana kumbakiza Walker

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester City imempa ofa ya mkataba mpya beki wa England, Kyle Walker ili kujaribu kumshawishi abaki katika klabu hiyo msimu huu wa majira ya joto, kwa mujibu wa 90minutes.

Walker ameingia katika miezi 12 ya mwisho ya mkataba wake wa sasa na amekuwa akilengwa na Bayern Munich, ambao wanatazamiwa kufanya mabadiliko katika beki ya kulia huku Benjamin Pavard akitaka kuondoka pale Allianz Arena.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, bado hajafanya uamuzi kuhusu mustakabali wake. Kuachwa nje ya kikosi cha kwanza kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya inaeleweka kumuumiza Walker na kuzua maswali juu ya kuendelea kwake hapo Manchester.



City wanatamani kumuona Walker akifanya uamuzi hivi karibuni na wanatumai kuwa beki huyo mkongwe atachagua kubaki.

Vyanzo vimeiambia 90min kwamba wameongeza ofa ya mkataba mpya kwa Walker ili kujaribu kumbakiza.

Walker ndiye anayepewa kipaumbele na Bayern katika nafasi yake ya beki wa kulia ingawa miamba hao wa Bundesliga bado hawajakataa ofa mpya ya mchezaji mwenza wa City, Joao Cancelo, ambaye walitumia miezi sita iliyopita.

Pia Walker ana ofa kutoka Saudi Arabia, lakini mchezaji huyo wa zamani wa Tottenham anaamini kuhamia Mashariki ya Kati kunaweza kuharibu nafasi yake kwenye kikosi cha England kwenye Euro 2024.

# Inter Miami kumsajili Alba

**MILAN, Italia**

VYANZO vimeitonya 90minutes kwamba, Jordi Alba, atajiunga na Inter Miami kwa uhamisho wa bure, akiungana na wachezaji wenzake wa zamani wa Barcelona, Lionel Messi na Sergio Busquets.

Timu hiyo ya Ligi Kuu ya soka ya Marekani, ilianza kumfuatilia raia huyo wa Hispania wiki kadhaa zilizopita, baada ya Alba kuthibitisha kuondoka Barcelona kutokana na kumalizika kwa mkataba wake.

Anaondoka Barcelona akiwa amecheza mechi 459 kwa jina lake katika kipindi cha miaka 11.


Ndiye mchezaji wa hivi karibuni atakayesajiliwa Inter Miami, ambao wameamua kurekebisha orodha yao wakati wa dirisha la uhamisho.

Kwa mara ya kwanza walimtangaza Lionel Messi mnamo Juni 7, baada ya mchezaji huyo kufichua dhamira yake ya kuichezea timu hiyo.

"Nilifanya uamuzi kwamba nitaenda Miami," alisema Messi.

Inter Miami walithibitisha kuwasili kwa Sergio Busquets wiki chache baadaye, kabla ya kumtangaza Gerardo 'Tata' Martino kuwa kocha mkuu wao mpya zaidi.

Watatu hao walicheza pamoja katika Ligi Kuu Hispania, LaLiga, kuanzia mwaka 2012 hadi 2021, wakishinda mataji matano ya ligi, sita ya Copa del Rey na moja la Ligi ya Mabingwa Ulaya.



HABARI MICHEZO

# AZAM YAPAA TUNISIA KUANZA KAMBI




**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha watu wasiopungua 40, wakiwamo viongozi, benchi la ufundi, wafanyakazi na wachezaji wa Azam FC, kimeondoka jana mchana jijini Dar es Salaam, kuelekea nchini Tunisia kwa ajili ya kuweka kambi ya maandalizi ya msimu ujao wa mashindano mbalimbali.

Ofisa Habari Msaidizi wa klabu hiyo, Hasheem Ibwe, amesema kikosi hicho kimeondoka jana Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA), kikipitia Dubai, kabla ya safari ya kuelekea jijini Sousse ambako ndiko kitakapokita kambi yake hadi kitakaporejea Julai 30.

"Mazoezi yalikwishaanza, lakini maandalizi makubwa na ya mwisho yanakwenda kufanyika nchini Tunisia ambako timu imechagua kuweka kambi kwa mwaka huu, kuna msafara wa watu wasiopungua 40 kwenye safari nzima, wakati huo huo kuna baadhi ya watu wapatao sita ambao wameshatangulia kwenye mji wenyewe ili kuweka mazingira sawa kwa ajili ya kambi hii," alisema Ibwe.

Alisema wanaamini wakiwa huko, Kocha Mkuu Msenegal, Youssouph Dabo, atapata fursa ya kukisuka kikosi hicho kwa ajili ya mashindano yanayowakabili.

"Tunategemea kutengeneza kikosi kizuri kitakachokuwa na mwanzo mzuri kwenye michezo ya Ngao ya Jamii, lakini kama haitoshi pale tutakapoanza harakati za ubingwa wa Tanzania Bara, Kombe la FA na michuano ya kimataifa msimu ujao," Ibwe alisisitiza.

Azam imeonekana kujizatiti kuelekea msimu ujao ambapo mbali na michuano ya ndani, itacheza pia Kombe la Shirikisho barani Afrika.

Imefanya usajili wa wachezaji wanne mpaka sasa ambao ni viungo washambuliaji, Feisal Salum na Djibril Sillah raia wa Gambia, straika Alassane Diao, na beki wa kushoto Cheikh Tidiane Sidibe kutoka Teungueth ya Senegal.

## Simba yashusha 'Ukuta wa Yeriko'

INATOKA UK. 24

Essomba na Kouame wote wana uwezo wa kucheza winga zote mbili, pamoja na nafasi ya mshambuliaji msaidizi, namba 10.

Che Fondoh amesajiliwa ikiwa ni siku chache baada ya klabu hiyo kumtoa kwa mkopo beki wake, Joash Onyango, huku pia ikiwa imempa mkono wa kwa heri beki raia wa Burkina Faso ambaye hakuwa sehemu ya kikosi cha kwanza, Mohamed Ouattara.

Kusajiliwa kwa wachezaji hao kumeamsha hamasa kubwa kwa mashabiki wa timu hiyo wakiamini kikosi chao kinaweza kufanya vizuri msimu ujao kwenye michuano ya kimataifa, Africa Super League Ligi ya Mabingwa Afrika pamoja na ile ya ndani Ligi Kuu Bara na Kombe la FA.

Msimu uliopita Simba ilishindwa kutwaa taji la Ligi Kuu kwa mara ya pili mfululizo huku ikipoteza ubingwa wake wa Kombe la FA, jambo ambalo wachambuzi na wataalamu wa soka nchini wabainisha ni kutokana na kukosa wachezaji wa akiba katika benchi wenye ubora sawa ama unaokaribiana na wale wa kikosi cha kwanza.

Hata hivyo, licha ya kushindwa kutwaa taji lolote, huku kwa upande wa Ligi Kuu ikimaliza nafasi ya pili, ilitoa wachezaji sita kwenye kikosi bora cha msimu, wakati katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika ikiishia hatua ya

# Mashabiki Simba watulizwa kwa Baleke

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Simba umesema mshambuliaji wao, Jean Baleke, ataungana na kikosi cha timu hiyo baada ya kwenda kwao kufuatilia hati mpya ya kusafiria (Passport) kutokana na ile ya awali kujaa.

Kulitokea taharuki kwa mashabiki wa Simba huku wale wa Yanga wakifurahia baada ya taarifa za mshambuliaji huyo kuondoka ghafla nchini kurejea kwao.

Baleke alitumia ukurasa wake wa mtandao wa kijamii akiweka picha akiwa kwenye ndege na kuandika 'Bye Bye' Tanzania na kuzua taharuki kubwa kwa Wanasimba.

Simba inatarajia kuondoka nchini kesho (Jumanne), kueleka nchini Uturuki na wachezaji wao wote waliowasajili kwa ajili ya maandalizi ya msimu wa 2023/24 wa mashindano.

Akizungumza na Nipashe jana, Meneja Idara ya Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally, alisema mchezaji huyo ameondoka jana kuelekea kwao kwa ajili ya kufuatilia hati ya mpya ya kusafiria.

Alisema anaona watu wanafurahia taarifa za kuondoka kwa Baleke, lakini atarejea ndani ya siku mbili hizi na kujiunga na timu kuelekea nchini Uturuki.

"Naona kuna watu wanataka kusikia kuwa mshambuliaji huyo ameondoka mazima, niwaambie tu kama tukiamua kumwondoka Baleke, wao wataathirika zaidi tutamchukuwa huyo Mkongo (Fiston Mayele) mwenzie aje kuziba nafasi yake (alitania).

"Sasa jukumu lao kumwombea dua Baleke aweze kupata haraka passport yake na arudi kazini mapema kuiwahi programu ya mwanzo wa maandalizi ya Preseason kuelekea msimu ujao," alisema Ahmed.

Aliongeza kuwa wameamua kufanya usajili mzuri na kuhakikisha wanaendelea kuimarisha kikosi chao kwa kuleta wachezaji ambao watasaidia timu kufikia malengo yao msimi ujao.



Baleke

## Yanga yaanika sababu kuweka kambi Bongo

INATOKA UK. 24

gida Fountain Gate nayo ambayo awali ilidai ingekwenda kuweka kambi nchini Tunisia, imeamua kubaki, ambapo sasa itakwenda kufanya 'preseason' yake Arusha.

Azam FC ilitarajiwa kupaa jana kwenda nchini Tunisia kuweka kambi, wakati Simba inatarajiwa kuondoka nchini kesho kuelekea Uturuki kwa ajili ya maandalizi ya mashindano ya kitaifa na kimataifa msimu ujao.

Wakati huo huo, klabu hiyo imesema hali ya mchezaji wake, Denis Nkane inaendelea vema baada ya kufanyiwa uchunguzi na kupata matibabu.

Kamwe amesema Nkane amepatiwa matibabu na sasa hali yake ni nzuri, hivyo kuwataka wanachama na mashabiki wa timu hiyo kutokuwa na wasiwasi.

Mchezaji huyo aliumia nchini Malawi wakati wa mechi ya kuadhimisha miaka 59 ya uhuru ya nchi hiyo, Yanga ilipocheza dhidi ya Nyasa Bullets, Uwanja wa Bingu wa Mutharika jijini Lilongwe Alhamisi iliyopita, timu hizo zikitoka suluhu.

# Michezo

Jumatatu Julai 10, 2023

Nipashe





De Gea atoa ujumbe mzito akiaga UTD UKURASA 21




Che Malone. **PICHA: SIMBA**

# SIMBA SC YASHUSHA ‘UKUTA WA YERIKO’

## ●●●Ni MVP wa pili akitokea Cameroon, fundi wa kukaba na kuchezea mpira kama Inonga, yasema sasa...

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imeendelea kujiimarisha katika dirisha hili kubwa baada ya kutangaza usajili wake wa tatu mpya msimu huu, safari hii akiwa na beki wa kati, Che Fondoh Malone, akitokea Coton Sport FC ya nchini kwao, Cameroon.

Taarifa iliyotolewa jana mchana na klabu hiyo imeeleza imemsajili mchezaji huyo katika kile kilichoeleza ni zoezi la kuboresha na kuimarisha kikosi chao kwa msimu mpya wa mashindano ya kitaifa na kimataifa, ikiwamo kurejesha mataji yao ya Ligi Kuu Tanzania Bara na Kombe la FA.

“Tumemsajili kwa mkataba wa miaka mwili kutoka Coton Sport na amekuwa ni nahodha wa kikosi hicho na kucheza mechi karibia zote za Ligi Kuu, Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho, ni mchezaji mwenye uzoefu mkubwa hasa kwenye michuano ya kimataifa na tunaamini atakuwa msaada mkubwa kikosini,” ilieleza taarifa ya klabu hiyo.

Che Malone (24), ambaye anajulikana kwa jina la utani ‘Wall of Jericho’ (Ukuta wa Yeriko), ndiye mchezaji bora wa Ligi Kuu nchini Cameroon (MVP) msimu wa 2022/23, akiitwa kwenye kikosi cha Timu ya Taifa ya Cameroon ‘Indomitable Lions’ pamoja na timu inayoshiriki michuano ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani, CHAN.

Aidha, Malone ambaye ana ubora wa hali ya juu katika ukabaji huku akijua kuchezea mpira kama alivyo beki wa Simba, Mkongomani Henock Inonga, anakuwa mchezaji wa tatu kutambulishwa rasmi na klabu hiyo, ambapo tayari wachezaji wawili, Mcameroon mwenzake, winga Wlly Essomba Onana aliyekuwa wa kwanza, akitokea Rayon Sport ya Rwanda ambaye naye alikuwa mfungaji bora kwenye ligi anayochezea akipachika mabao 16 na ‘assist’ tano na kuwa MVP wa msimu uliomalizika.

Mchezaji mwingine ni raia wa Ivory Coast, Aubin Kramo Kouame (27), akitokea Asec Mimosas ya huko, aliyefunga mabao matatu kwenye mechi tatu za Ligi ya Mabingwa Afrika na manne Kombe la Shirikisho Afrika katika mechi 10 ambazo timu yake imecheza msimu uliopita na kuishia nusu fainali.


UKURASA. 23


# Yanga yaanika sababu kuweka kambi Bongo

**Na Adam Fungamwango**

HATIMAYE Klabu ya Yanga imetangaza rasmi kuwa kambi yake ya maandalizi kwa msimu wa mashindano 2023/24 itakuwa nchini Tanzania, huku baadhi ya wachezaji wake wakitarajiwa kuwasili leo.

Awali, kulikuwa na hatihati kuwa kikosi cha timu hiyo kitafanya ‘preseason’ yake hapa nchini au nje ya nchi, huku Ofisa Habari wake, Ali Kamwe, akisema atawatangazia vyovyote vile itakavyoamuliwa.

Meneja wa timu hiyo, Walter Harrison, amesema jana kuwa ‘preseason’ ya kikosi hicho cha Mabingwa wa Tanzania Bara itakuwa nchini jijini Dar es Salaam kama ilivyokuwa msimu uliopita kwa sababu mbalimbali, ikiwamo ufinyu wa muda, pamoja na kumpa nafasi Kocha Mkuu, Miguel Gamondi kuzoea mazingira na hali ya hewa ya hapa nchini.

“Wachezaji wetu wataanza kuwasili tarehe 10, baada ya hapo tutaanza ‘preseason’ ambayo tutaifanyia hapa nchini, jijini Dar es Salaam kama ilivyokuwa msimu uliopita, hii inatokana kuwa na ufinyu wa muda kuweza kujiandaa hatimaye kurudi kujiandaa na Tamasha la Mwananchi, baada ya hapo tunakwenda kwenye mechi za Ngao ya Hisani kule Tanga,” alisema Harrison.

Alisema ratiba yao imekuwa ngumu kiasi kwamba imewafanya kushindwa kutoka nje ya Dar, lakini akawatoa hofu wanachama na mashabiki wa timu hiyo kuwa watakuwa kwenye kambi yenye vifaa bora vya kuwawezesha kufanya aina yoyote ya mazoezi na maandalizi ambayo wanataka kuyafanya.

“Kambi yetu ina vifaa bora vya kuwezesha aina yoyote ya maandalizi ambayo sisi tunataka kuyafanya, ndiyo maana tumeamua kubaki hapa hapa, lakini vile vile ni wasaa mzuri pia kocha wetu kuzoea mazingira ya hapa pamoja na hali ya hewa ya nchini ili kumwezesha kufanya maandalizi yaliyo bora kabisa kwa msimu ujao ambao pia tunatamani kuweka tena historia na kuendelea kuwapa raha wanachama na mashabiki wa Yanga,” alisema meneja huyo.

Wakati Yanga ikibakia nyumbani, Sin-


UKURASA. 23



GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042


9 770856 541002 >